USHIRIKISHAJI WANAWAKE KATIKA UONGOZI

KITINI CHA MWONGOZO WA MAFUNZO

Waandishi
Asha Aboud
Hawra Shamte

Januari, 2019
Kimefadhiliwa na UN WOMEN

JUWAUZA

YALIYOMO

Vifupisho ii

Shukran iii

Utangulizi 1

Kwa nini tuangalie ushiriki wa wanawake katika siasa.....2

Malengo ya mwongozo 3

Mbinu shirikishi zitakazotumika kufundishia 4

Moduli ya 1: Dhana muhimu za Jinsia 8

Moduli ya 2: Haki ya Wanawake Kushiriki katika Siasa 20

Moduli ya 3: Jamii na Uongozi wa Wanawake.....25

Moduli ya 4: Wajibu wa Wadau 34

Marejeo 39

VIFUPISHO

BLW	Baraza la Wawakilishi
CEDAW	Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake
JUWAUZA	Jumuiya ya Wanawake wenye Ulemavu Zanzibar
JUMAZA	Jumuiya ya Maimamu Zanzibar
SADC	Shirika la Maendeleo la Kusini Mwa Afrika,
SUZA	Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar
MKUKUTA	Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania
MKUZA	Mpango wa Kukuza Uchumi na kupunguza umasikini Zanzibar
PPC	Klabu ya Waandishi wa Habari Pemba
TAMWA, ZNZ	Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Zanzibar
UWAWAZA	Umoja wa Wawakilishi Wanawake Zanzibar
UN	Umoja wa Mataifa
URT	Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
VICOBA	Banki za Kijamii
ZAFELA	Chama Cha Wanasheria Wanawake Zanzibar
ZYF	Jukwaa la Vijana Zanzibar
ZU	Chuo Kikuu cha Zanzibar

Shukran

Kuandaa mwongozo wa mafunzo kuhusu ushirikishaji wanawake katika nafasi za uongozi wa kisiasa ni kazi iliyohitaji kuwashirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo na watetezi wa haki za binadamu. Hivyo mwongozo huu ni matokeo ya juhudi zisizo na kifani za watu binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali ya watetezi wa haki za wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto Zanzibar pamoja na vyama vya siasa. Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) Zanzibar kinapenda kutoa shukrani za dhati kwa wale wote waliotoa mchango wao katika kazi hii.

Shukrani za kwanza kabisa zinakwenda kwa Shirika la Wanawake la Umoja wa Kimataifa UN WOMEN kwa msaada wao mkubwa wa kifedha uliowezesha kazi hii kufanyika. Tunatambua na kushukuru mchango wa kitaalamu uliotolewa na mkufunzi Bi Rukia Mohamed Issa wa Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU), Bw Salum Ali wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Bi Salma Saadat mwenyekiti Umoja wa Walemavu, Bi Khadija Hassan kutoka Chama Cha Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), Bw Mohamed Jabir kutoka Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Maalim Ali Haji Ubwa kutoka Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA), Bi Najma Khalfan Mwandishi mkongwe wa SWAHIBA FM, Abdallah Ali Abeid Mkurugenzi Mtendaji wa Jumuiya ya Kupambana na Changamoto za Vijana, Zanzibar (ZAFAYCO), Ali Sultan ambaye ni mwandishi mtafiti wa kujitegemea na Zeudi Abdillahi kutoka Jukwaa la Vijana Zanzibar (ZYF).

Kwa kuwa si rahisi kuwataja wote waliochangia mawazo katika kukiimarisha muongozo huu, tunawaomba wote kwa ujumla wao wapokee shukrani zetu za dhati.

Mwisho, TAMWA Zanzibar inawashukuru wote ambao walitoa mchango wao kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha uandaaji wa kitini hiki cha mwongozo wa kufundishia ili jamii ivae miwani ya kijinsi na kumuona mwanamke kama mshiriki mwenza katika maendeleo hivyo kupata nafasi ya uongozi ni haki yake ya kikatiba, ya kitaifa, ya kimataifa na hata ya kidini.

Dr Mzuri Issa
Mkurugenzi
TAMWA (Zanzibar)

Ushirikishwaji wa jamii kuwapa wanawake nafasi za uongozi

1.0: UTANGULIZI

Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ina visiwa viwili; Unguja na Pemba ambavyo vina jumla ya wilaya 11; saba Unguja na nne Pemba. Katika sensa ya mwaka 2012 Zanzibar ilikuwa na wakazi 1,300,000. Kati ya hao wanawake wanaakisi 51% ya watu wote (Laura 1994). Pamoja na wingi wao lakini wanawake mara nyingi wamekuwa wakitengwa kutokana na mitazamo ya kihistoria na kijamii. Kwa muda mrefu wanawake wa Zanzibar walikuwa hawaruhusiwi kushiriki katika nyanja za kisiasa.
Ni mwanamke mmoja tu mwafrika Christabel Majaliwa, ambaye mwaka 1960 aliteuliwa kuwa mjumbe asiye rasmi katika Baraza la Kutunga Sheria tangu lilipoanzishwa mwaka 1914. Huyo alikuwa ni mmoja kati ya wajumbe 67. (Fair, 1994, p.69).

Mpaka hivi leo nafasi ya mwanamke katika ulingo wa kisiasa haijabadilika sana kwani bado idadi yao ni ndogo katika ngazi za maamuzi. Mambo mengi yameainishwa kuchangia hali hiyo ikiwa ni pamoja na mfumo dume, mila na desturi, dini, viwango duni vya elimu, kutokujiamini, wanaume kuhodhi nafasi za uongozi katika vyama vya siasa, mazingira yasiyo maridhawa ya sheria za uchaguzi pamoja na gharama kubwa na kuendesha uchaguzi.

Tanzania ina utaratibu wa kufanya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge, Wawakilishi na Madiwani kila baada ya miaka mitano. Kwa kawaida nafasi ya wanawake katika chaguzi hizi bado ni finyu sana pamoja na kuwa dhamira ni kufikia asilimia 50 kwa 50. Katika uchaguzi wa mwisho (2015) idadi ya wanawake waliopata nafasi za uongozi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Jimboni, Viti maalum na Uteuzi wa Rais ilikuwa ni 126 kati ya wabunge 393 sawa na asilimia 32.

Kwa Zanzibar wanawake walioingia katika Baraza la Wawakilishi ni asilimia 36 (36%) ambao ni jumla ya wawakilishi 28 kati ya 84. Wanawake waliopata nafasi za udiwani ni 85 kati ya 173, ikiwa ni sawa na 49%. Kulingana na takwimu hizo bado wanawake hawajapata fursa sawa kijinsia katika utawala na utoaji maamuzi katika Bunge, Baraza la Wawakilishi na kwenye Halmashauri.

Ni muhimu kuweka bayana kuwa idadi hiyo imefikiwa pia kutokana na kuwepo kwa viti maalum na kwamba ieleweke kuwa viti hivyo ni kwa ajili ya mkakati wa dharura tu, lengo ni ifikie wakati wanawake waingie katika ngazi za mamuzi kupitia kugombea majimboni. Hadi sasa asilimia ya wanawake wanaopata nafasi kupitia majimboni ni ndogo sana na bado siasa kwa ujumla wake imetawaliwa na mfumo dume. Ni wanawake saba tu ndio walioshinda viti vya uwakilishi kupitia majimboni kati ya majimbo 54 yaliyopo hiyo ni sawa na asilimia 13 (13%). Kwa upande wa madiwani ni wanawake 23 tu walioshinda kupitia uchaguzi kati ya viti 111 vilivyopo ikiwa ni sawa na asilimia 20 (20%). Wakati wanawake walioshinda viti vya ubunge kutoka Zanzibar ni watatu tu kutoka majimbo 50 yaliyopo Zanzibar ikiwa ni sawa na asilimia 6 tu (6%).



Kulingana na takwimu hizo bado wanawake hawajapata fursa sawa kijinsia katika utawala na utoaji maamuzi Bungeni, kwenye baraza la wawakilishi na kwenye Halmashauri. Ni kutokana na mapungufu haya ya kihistoria ndipo wanaharakati wanapojenga hoja ya 50/50 ili kuongeza na kuweka uwiano sawa kati ya wanawake na wanaume katika nyanja zote za uongozi.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka bayana haki za wanawake za kushiriki katika uongozi. Ibara ya 21 inasisitiza kuwa kila raia wa Jamhuri ya Muungano ana haki sawa za kushiriki katika uongozi wa nchi aidha moja kwa moja au kwa njia ya uwakilishi. Tanzania haiwezi kupigana na umaskini, wala kuimarisha demokrasia bila ushiriki wa wanawake katika nyanja zote za maamuzi ikiwa ni pamoja na ushiriki wao katika vyombo vyote vya uwakilishi kuanzia ngazi ya Kata, Jimbo hadi Taifa (URT:1998).

Sehemu ya 21 ya Katiba ya Zanzibar pia inaeleza kwamba kila mtu apewe nafasi sawa katika kupata nafasi za uongozi kwenye serikali, aidha kwa njia ya moja kwa moja ama kupitia wawakilishi wao waliochaguliwa kwa njia huru na haki. Hivyo, hatuwezi kusema kuwa tunazingatia usawa wakati wanawake ambao ndio wengi nchini hawashirikishwi ipasavyo katika ngazi za maamuzi.

2.0: Kwanini tuangalie na kuzungumzia wanawake kuingia katika ulingo wa siasa na vyombo vya kutunga sheria

Nchi kutekeleza misingi ya demokrasia kunahitaji kuwepo na mikakati iliyo imara ya kuona kuwa kunakuwepo na ushiriki wa watu wote katika mijadala inayohusu masuala ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na masuala mengine muhimu kwa maendeleo ikiwa ni pamoja na kushika nafasi za uongozi katika ngazi mbali mbali katika vyama vya siasa na katika utawala. Na ushiriki maana yake ni pamoja na kushirikishwa katika michakato yote ya utoaji wa maamuzi. Katika vyama vya siasa na katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Hivyo basi; wanawake wanavyoshajiika kuwa viongozi wa kisiasa, uzoefu kutoka katika nchi nyingi unaonyesha kuwa kunakuwa na maisha bora na maendeleo na hii imejionyesha katika sekta ya elimu, afya na katika sekta nyenginezo. Wanawake wanavyoshiriki kikamilifu katika nyadhifa

wanazopewa huleta mabadiliko katika jamii, kwenye vyombo vya sheria, vyama vya siasa na hata kwa maisha ya wananchi.

Tafiti mbali mbali zimeonyesha ushiriki wa wanawake katika siasa huleta matokeo chanya katika kufikia utawala wa kidemokrasia pamoja na kushughulikia masuala ya wananchi, kuongeza ushirikiano miongoni mwa vyama vya siasa na kuimarisha uendelezaji/uimarishaji wa amani.

Wanawake hujikubalisha kujenga amani na usalama na kujenga mifumo ya maridhiano baada ya kutokea migogoro, kuweka mitazamo ya kimadaraka katika meza za maridhiano. Tafiti pia zimeonyesha ujengaji wa makubalianao ya amani, maridhiano na utawala wa sheria hupata mafanikio wanaposhirikishwa wanawake (Chinkin, 2003)

Imethibitishwa na wanazuoni kuwa na jamii yenye amani na utulivu kunahitaji mageuzi ya mahusiano ya madaraka ikiwa ni pamoja na kuweko na usawa wa mahusiano ya kijinsia (Strickland and Duvvury, 2003).

Wanawake wanavyochaguliwa katika vyombo vya kutunga sheria hutetea kuweko na sera zenye vipaumbele vya masuala ya familia, wanawake na makundi yaliyo pembezoni au yenye mahitaji maalum. Ni muhimu kwa wanawake kuwa wengi katika vyombo vya utawala ili kuwakilisha mahitaji ya wanawake na wapiga kura wa makundi yenye mahitaji maalum na kupendekeza sera mbadala. Kwa kawaida wanawake hupendelea kufanya kazi kwa mashirikiano na makubaliano kulinganisha na wanaume na hii ni miongoni mwa mbinu mojawapo katika kufikia demokrasia ya kweli.

Hata hivyo wanawake huwa hawapati nafasi za uongozi kutokana na jamii kuweka mgawanyo wa kazi kwa mujibu wa jinsia (gender roles) ambazo humfanya ashughulike na kazi tu za ndani ambazo huwa nyingi mno na zile za nje ambazo hazina kipato na mwanamme kushughulika na kazi za nje tena zenye kipato. Wanawake wana kazi za aina tatu (Triple roles):

1) ***Kazi ya uzazi—***Hizi ni kazi za kuzaa watoto, kuhudumia watoto, baba, wageni, wagonjwa na nyumba kwa ujumla.

2) ***Kazi ya uzalishaji*** **-** Hizi ni kazi ambazo wanawake huzifanya kwa ajili ya familia ikiwemo kuzalisha mazao ya chakula na hata biashara ili kukidhi mahitaji ya nyumbani.

3) ***Kazi za kijamii***-Hizi ni kazi ambazo wanawake huhusika nazo kama sehemu ya jamii zikiwemo harusi, maziko, miradi ya kimaendeleo, kampeni za kisiasa na kupambana na vitendo vya udhalilishaji.

4) Kutokana na majukumu haya mengi, mwanamke hukosa muda wa kushughulika na shughuli za kushiriki katika siasa akiwa mgombea. Hivyo jamii inahitaji kuyaelewa haya na kuona ni jinsi gani inaweza kumweka mwanamke katika sehemu mahususi ili ashiriki kwenye siasa kama mgombea.

MUNAISHIJE HAPA? JE WANAWAKE WANAFANYA KAZI?
HAPANA HATUFANYI KAZI ...TUPO TUPO TU NYUMBANI...
...TUNACHOTA MAJI, KUTAFUTA KUNI, NA KUANGALIA MIFUGO...
...TUNAANDAA BUSTAN PAMOJA NA KUPANDA MBEGU...
...NA TUNAPALILIA KISHA TUNAVUNA MAZAO, NA KUYAUZA SOKONI....
...TUNANUNUA CHAKULA SOKONI, KUPIKA NA KUFANYA KAZI ZA NYUMBANI...
...TUNASHIRIKI MIKUTANO YA KINA MAMA KWA AJILI YA SHUGHULI ZETU ZA VIKUNDI KAMA VILE - KUTENGENEZA MATOFALI KWA AJILI YA UJENZI WA SHULE...
...KUFUA NA KUSHONA NGUO ZA WATOTO TUNAWALEA NA KUWAKUZA... TUNAHUDUMIA WAGENI NA WAGONJWA... NI HAYO TUUU.....
...KWA HIVYO, HAPANA, HATUFANYI KAZI !
MMM... NILITAKA KUANGALIA TUU!

2.1: **Malengo ya mwongozo**

Madhumuni ya kitini hiki ni kutoa mwongozo kwa wahusika wa kijamii katika kuhamasisha makundi mbali mbali juu ya kumuona mwanamke kama ni mshiriki halali wa masuala ya kisiasa.

2.2: Matarajio

Mwisho wa mafunzo washiriki waweze kufanya yafuatayo:

- Kufahamu umuhimu wa uongozi wa wanawake katika siasa kwenye ngazi ya wadi, jimbo na Taifa.

- Kuainisha masuala muhimu ambayo yatasaidia wanawake kufanikiwa katika chaguzi za wadi, majimbo na Taifa

- Kuonyesha na kutoa mifano ya ufahamu ya nafasi na majukumu ya wadau mbali mbali katika kusaidia wanawake wanaogombea nafasi za uongozi katika wadi, jimbo na Taifa.

2.3: Mambo ya kuzingatia kwa wakufunzi

2.3.1 Wawezeshaji kabla ya kuanza kufundisha watakiwa kufanya yafuatayo ili mafunzo yaweze kufanikiwa na kuleta tija;

- Kabla ya uwasilishaji wa moduli yoyote, mwezeshaji atatakiwa kuisoma na kuifahamu vyema.
- Kuandaa darasa la kufundishia – liwe linafikika na mazingira yawe rafiki
- Mwezeshaji afahamu mahitaji ya wale anaowafundisha
- Mwezeshaji atatakiwa kujitayarisha na kujiweka sawa kwa kuhakikisha anavyo vifaa muhimu vya kufundishia na vya kujifunza pamoja na nyenzo ya tathmini.
- Kuandaa vikundi vya majadiliano kwa kuzingatia jinsi, jinsia, umri na mchanganyiko wa uzoefu.
- Mwezeshaji atatakiwa kuzingatia ukubwa wa kundi (darasa lisizidi watu 25) ili kuwezesha mazingira mazuri ya ushiriki kwa kila mwanakikundi.
- Mwezeshaji atakapotoa kazi za vikundi anatakiwa ahakikishe anafanya ufuatiliaji wa karibu kwa ajili ya kutoa mwongozo na msaada iwapo utahitajika.
- Mwezeshaji atatakiwa kujitahidi kuchota uzoefu walionao washiriki na kuutumia uzoefu huo katika kutoa mifano na kuongeza mbinu za kufundishia
- Mwezeshaji atumie lugha ya ishara ili aeleweke vizuri (body language)
- Mwezeshaji atatakiwa kutambua kuwa washiriki ni watu wazima hivyo anapaswa kuwaheshimu na kutumia lugha itakayowajenga na kuwapa moyo. Ni muhimu kutumia mbinu shirikishi kwani hiyo itasababisha washiriki kupenda kujifunza na kushiriki mafunzo kwa uchangamfu na ukamilifu. Muda mchache mwezeshaji anaweza kutumia njia ya kutoa muhadhara kwa kuweka hali ya utayari wa kupokea mafunzo.

Katika uwezeshaji ni vyema kuwepo ufuatiliaji wa mitazamo ya washiriki katika kushirikisha, kugombea na kuchaguliwa kwa wanawake katika nafasi mbali mbali za uongozi katika wadi, majimbo au Taifa. Hili ni eneo muhimu kuliangalia kwani litawezesha kufahamu na kutambua kama lengo la mafunzo limefikiwa.

3.0: Mbinu shirikishi za ufundishaji

3.1: Hotuba

Njia hii hutumika kutoa mada au somo la kitalamu kwa walengwa kwa kutoa hutuba. Njia hii itatumika kwa kutayarisha masomo yenye mada mbali mbali zitakazo wasilishwa katika mafunzo za kuwaelimisha wanawake katika ulingo wa siasa na uongozi

3.2: Changamsha bongo

Mbinu hii hutumika kuwataka walengwa kuchangia mada na itatumika kabla ya mada kuwasilishwa kwa kuwapima walengwa ufahamu wao na michango walionao ili kuleta ufanisi wa mada husika

3.3: Kazi za vikundi

Njia hii ni ya kusoma kwa pamoja ambayo inafanywa na wana kikundi kuchangia katika kazi au mada iliyotolewa ili kufanya mchakato wa mafunzo kuwa bora. Njia hii huwapa uhuru wa shiriki na kutoa fursa kwa wale ambao hushindwa kuzungumza katika kundi la watu wengi, njia hii inashajihisha mfumo mzuri wa kujifunza na ufahamu.

3.4 Majadiliano na midahalo

Njia hii hufanyika kwa kutolewa kichwa cha habari cha mada na kutakiwa washiriki kujadiliana kwa kutoa hoja za msingi na baadaye kufikia mwafaka. Hii inasaidia washiriki kubadilishana uzoefu na mawazo. Mdahalo pia ni mbinu inayoweza kutumika katika kufundishia kwa kuwataka washiriki kufanya mazungumzo baina yao hasa zile mada zenye matatizo au utata. Njia hii inaweza kutumika wakati wa kujadili mila zinazo athiri nafasi ya mwanamke katika siasa na utatuzi wake.

3.5 Maigizo

Hii ni njia ya ufundishaji kwa kutumia maigizo ambayo walengwa husoma/kujifunza kwa kuigiza uhusika wa tatizo fulani na hadhira hupata uelewa mkubwa

3.6: Uwasilishaji wa mada

Njia hii hutumika zaidi iwapo jambo linalotaka kuwasilishwa ni jambo jipya au linafikiriwa jambo ni geni kwa washiriki. Mada hutayarishwa na kuwekwa kwenye kitini au huwasilishwa kwa kutumia nguvu nukta (power point). Njia hii itatumika katika kutoa maarifa mapya juu ya usawa wa kijinsia.

3.7: Utoaji hadithi

Hii ni njia kusimuliana hadithi za kuelimishana juu ya jambo fulani. Kila mlengwa anaweza kutoa uzoefu wake kuhusu mada inayotaka kuwasilishwa. Walengwa wataweza kutoa maelezo yao juu ya tatizo au jambo linalozungumzwa kwa kuelimishana kwa kuonyesha namna wanawake wanavyopewa nafasi za uteuzi.

3.8: Visa mafunzo (Case studies)

Njia hii inatumika kutoa taarifa ya jambo Fulani ikiwa kma nikukazia kwa kutoa hali iliopo ili washiriki kufahamu jambo linalozungumzwa kwa mifano hai kabisa. Njia hii itatumika katika kutoa uzoefu wa wanawake katika kutangaza nia, kuteuliwa, takuwimu za wagombea, za wapiga kura na hata mikutano ya kampeni.

Malengo ya Moduli ya 1.

Baada ya kumaliza sura hii washiriki wataweza:-

- Kuelewa kwa undani dhana za jinsia na kufanya uchambuzi wa kijinsia katika masuala yote yanayohusu uchaguzi.
- Kuelezea dhana potofu, mawazo mgando na usawa wa kijinsia
- Watafahamu mfumo dume na mapambano dhidi ya mfumo huo
- Wataelezea nafasi ya mwanamke katika demokrasia ya uchaguzi
- Pia kuelewa maana ya uongozi na sifa za uongozi
- kufanya uchambuzi na uhusiano wake katika mchakato wa uchaguzi na ngazi mbali mbali za utoaji maamuzi

MODULI YA 1
Dhana muhimu za Jinsia

1.0: Utangulizi

Nyanja ya jinsia na maendeleo ni uwanja wa kitaaluma wenye nadharia na nyenzo mahsusi za uchambuzi. Pia ni kigezo muhimu katika uchambuzi wa jamii iliyojengeka katika mfumo dume. Hivyo jinsia hujumuisha dhana na zana muhimu za kuchambua mifumo ya maendeleo.

Moduli hii inatoa maelezo mafupi juu ya dhana muhimu za jinsia kwa madhumuni ya kuwezesha wagombea wanawake, vijana na watu wenye ulemavu:

- Kuelewa kwa undani dhana za jinsia na zinavyohusiana na maendeleo hususan demokrasia na uongozi katika siasa.

- Kutoa ufafanuzi wa imani na fikra mgando juu ya dhana za jinsi na jinsia.

- Kujenga uwezo wa wagombea kwa kutumia dhana za jinsia kuchambua jinsi zinavyoweza kuwaathiri katika kinyang'anyiro cha uchaguzi.

Mbinu/mazoezi ya vitendo

Mwezeshaji ataanza Somo hili kwa kuwauliza washiriki kwa kutumia mbinu ya bunga bongo kutoa maana/ dhana ya maneno ya jinsi na maana ya jinsia kwa kuwataka waonyoshe mkono na kuelezea tafsiri ya maneno haya na baadaye kuonyesha tofauti zao.

Baada ya kutoa tafsiri na tafauti ya maneno, washiriki watatakiwa kuonyesha majukumu ya mwanamke na mwanamme kuanzia asubuhi wanavyoamka hadi muda wa kulala. Kueleza kazi gani anafanya zaidi mwanamke na kazi gani anafanya mwanamme katika ngazi ya familia, ngazi ya jamii na ngazi ya Taifa zoezi hili litafanyika kwa njia ya makundi.

Mwezeshaji ataongoza somo hili kwa kutumia uzoefu alionao juu ya mgawanyo wa majukumu katika ngazi zote kwa kutoa kazi za vikundi. Baada ya uwasilishaji wa kazi za vikundi mwezeshaji ataendelea na mada kwa kuelezea dhana za jinsia kuonyesha tofauti zao na kutoa mifano

2.0: Maelezo muhimu kuhusu dhana za jinsia na maendeleo

2.1. Jinsi na jinsia

Msingi Jinsi	Msingi Jinsia	Mwingiliano na Sera na programu
Maumbile ya kibailojia yanayotofautisha mwanamke na mwanaume	Mahusiano uwezo na mamlaka yaliyojengeka kati ya wanawake na wanaume katika jamii kwa kufuata misingi mila na desturi. Mahusiano hayo hutofautiana kati ya sehemu na sehemu na kulingana na muda na yana mwingiliano na rangi, makabila, tabaka na dini Mahusiano ya jinsia huweka misingi ya kugawa rasilimali na maamuzi	Kuwepo fikra potofu zinazohusisha majukumu, nafasi na hadhi ya wanaume na wanawake katika jamii na maumbile ya kibaiolojia mfano baadhi ya jamii kuwekea mashaka uwezo wa mwanamke kama kiongozi kwa sababu ya kuingia kwenye hedhi, na kubeba mimba
Mwanamke ameumbwa na maumbile yanayomwezesha kubeba mimba, kuzaa na kunyonyesha hivyo kubeba majukumu, ya kubeba mimba na kunyonyesha. Mwanamme ana maumbile ya mbegu za uzazi na hivyo kuwa na jukumu katika kutunga mimba Maumbile haya yanafanana kwa wanawake na wanaume wote duniani	Kuwepo na taasisi katika jamii zinazoendeleza makuzi na malezi yenye kujenga mahusiano ya jinsia zikiwepo familia, shule, taasisi za dini na sehemu za kazi Taasisi hizi husimamia mila na desturi zenye mtazamo hasi ambazo zinaleta mahusiano ya jinsia yasiyo sawa na kuwaweka wanaume katika nafasi za uongozi na mamlaka juu ya rasilimali na maamuzi.	Ni kutokana na maumbile tofauti wanawake na wanaume huwa na mahitaj tofauti ya afya mfano kwa wanawake wakati wa hedhi na uhitaji wa kuendesha kampeni ya kansa ya prostati na matiti.
Majukumu ya mwanamke ya kubeba mimba na kuzaa yanahitaji rasilimali ya muda wa mama. Pia yanahitaji kutambuliwa na jamii na mifumo husika ili kumwezesha kushiriki katika uongozi na		Sera za maendeleo lazima zibainishe mahitaji ya kijinsi na kuelekeza upatikanaji wa rasilimali na mahitaji hayo wanawake na wasichana kupatiwa pedi za kutumia wakati wa hedhi kwa bei nafuu. Pia wanawake kupatiwa

michakato mingine ya maendeleo. Aidha majukumu ya kibaologia ya mwanamke na mwanmke yanahitaji kupata huduma stahiki za afya		huduma ya uzazi salama wakiwa wajawazito na wakati wa kuzaa
Jinsi haibadiliki	Jinsia inabadilika	

2.2: Kazi/majukumu kijinsia

Majukumu na mgawanyo wa kazi kijinsia hutokana na mitazamo na mategemeo ya jamii kwa wanawake na wanaume hupelekea jamii kuainisha kazi/majukumu tofauti ya wanaume na wanawake kwa mujibu wa mategemeo ya jamii ambayo mara nyingi hujengwa juu ya mfumo dume, fikra mgando na mazoea katika jamii na taasisi zake.

2.2.1: Nini athari za mgawanyo wa kazi usio sawa kwa wanawake na watoto wasichana?

Unawabebesha wanawake majukumu zaidi na hivyo kuwapunguzia nafasi za kushiriki michakato ya maendeleo ikiwemo elimu na uongozi.

Wanawake wengi, hasa wa vijijini mara nyingi huwa na afya duni kwa sababu ya kazi nyingi wazifanyazo.

2.3: Mfumo dume

2.3.1: Nini maana ya mfumo dume?

Ni mfumo uliorasimishwa katika jamii wenye kuendeleza mifumo inayokandamiza, kunyonya na kuonea na inaendeleza kutokuwepo kwa usawa:

Mfumo dume umejengeka katika ngazi zote kuanzia kaya, jamii, taifa hadi kimataifa na unaendelezwa na sera, sheria na michakato na mikakati ya maendeleo ambayo kwa kiasi kikubwa husimamiwa na wanaume.

Mfumo huu hujidhihirisha zaidi kwenye madaraka na mamlaka ya kumiliki rasilimali; mifumo na mahusiano yasiyo sawa kati ya wanawake na wanaume, wanawake kwa wanawake na wanaume kwa wanaume na kati ya taasisi za nchi zilizoendelea na zinazoendelea.

Mfumo dume umejipenyeza na kujiingiza katika taasisi mbali mbali ikiwepo mifumo ya siasa, dini n.k. inayomweka mwanamme kama kielelezo cha kiongozi. Fikra hizi wakati mwingine zimepelekea kuona kuwa wanawake "hawafai" kuwa viongozi wa siasa. Hii imerudisha nyuma maendeleo ya wanawake katika nyanja ya siasa.

Pamoja na kuwa mfumo dume unaonekana kuwakandamiza zaidi wanawake, mfumo huu unapoangaliwa katika mapana, huathiri wanawake na wanaume.

Mfano: Inapotokea mfumo dume wa kibepari unamkandamiza mwanamme kwa kumwachisha kazi basi huathirika kwa kushindwa kutimiza wajibu wake wa kupatia familia yake mahitaji. Hapo mwanamke hulazimika kubeba jukumu la kutunza kaya.

2.4: Mawazo mgando

Ni nini maana ya mawazo mgando?

Mawazo mgando katika maisha ya jamii na jinsi mawazo hayo yameendeleza au kukwamisha maendeleo, au yamenyima demokrasia ya kweli au yamewatoa watu katika ushiriki wa maamuzi katika taifa.

Kwa ufupi mawazo mgando ni mtazamo au fikra zisizobadilika katika jamii na kuziona kila siku ni zile zile japo kuwa mitazamo/fikra hizo haziisaidii jamii katika kujikomboa. Ni fikra/mitazamo isiyojenga wala isiyotaka mabadiliko.

2.4.1: Jinsi ya kutambua mawazo mgando yanayoathiri maendeleo.

- Kudumaza maendeleo na harakati za wanawake katika Jamii.
- kutoshirikishwa kwa wanawake katika mipango na utekelezaji.
- Kutoshiriki katika masuala ya Maamuzi
- Kutumia uasili zaidi kuliko usasa katika masuala ya Jinsia.

2.5: Mahitaji ya kawaida ya kijinsia

Ni nini tofauti ya mahitaji ya kawaida na mahitaji mbinu?

Vidokezo vya mahitaji ya kawaida:

Yanampatia mwanamke mahitaji ya kumsaidia kuishi na kufanya kazi zake za kila siku – mfano; chakula, makazi, kuni, maji n.k. na kumwacha katika hali yake ya kawaida yaani kama ni maskini anabaki na hali hiyo hiyo.

Kumpatia mwanamke maji katika utaratibu wa kawaida wa kutoa huduma hakubadilishi utaratibu usio sawa wa mgawanyo wa kazi unaomwachia mwanamke na mtoto msichana kazi ya kuchota maji kwa matumizi ya nyumbani.

Aidha utaratibu wa kufikia mahitaji ya kawaida haumpi mwanamke uwezo wa kuhoji kwa nini jamii imeacha kazi nzito ya kuchota maji yenye adha kubwa kuwa ya wanawake tu?

Hata hivyo mahitaji ya kawaida kwa wanawake kuhakikisha maisha bora yenye kulinda utu wao. Mahitaji hayo yanahitaji kuzingatiwa na kupewa umuhimu katika sera, mipango na bajeti. Aidha ni muhimu kwa wanawake wapate fursa ya kushiriki michakato ya mipango na bajeti inayohusiana na upatikanaji wa mahitaji na kupatiwa nafasi za uongozi.

2.6: Mahitaji mbinu

Tofauti na mahitaji ya kawaida, haya ni mahitaji yanayowawezesha wanawake kuhoji misingi na mifumo inayopelekea kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia na mgawanyo wa kazi usio sawa; ubaguzi wa kijinsia na watu walio pembezoni; ukatili kwa wanawake n.k

Mahitaji mbinu yanaweza kutokana na wanawake kuwa na:

- Elimu ya sheria juu ya wanawake na haki za binadamu, hususani haki za kumiliki ardhi
- Elimu juu ya uzazi wa mpango na bora na umuhimu wa kuwa na maamuzi katika mahusiano ya ngono
- Elimu ya uongozi na mbinu za kutumia ili kushinda katika uchaguzi

- Wanawake kuanzisha vyama vya kuweka na kukopa (VICOBA) na mitandao ya kupambana na ukatili wa wanawake.

*Kama ilivyosisitizwa kwa mahitaji ya kawaida, mahitaji mbinu nayo yanatakiwa yaingizwe na kupewa umuhimu stahiki katika sera, mipango na bajeti.

2.7: Usawa wa kijinsia

Ni vipi vidokezo muhimu vya dhana hii?

Hali ambayo wanawake na wanaume wanapata fursa, mafao, haki wajibu sawa katika nyanja zote za maisha. Ni uwiano wa mgawanyo wa majukumu kati ya mwanamke na mwanamme.

Usawa kati ya mwanamke na mwanaume unapatikana pale ambapo jinsi hizi mbili zinapoheshimu haki za kila mmoja, kuthaminiana, kugawanya kwa usawa madaraka na mamlaka yaani kuwa na fursa sawa katika nyanja zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa na kufikia fursa za elimu na rasilimali kwa usawa.

2.7.1: Ni nini faida ya kuwapo kwa usawa wa jinsia?

- Kumwezesha mwanamke ili awe kiini cha kufikia usawa
- Kuwapa wanawake uwezo wa kutawala maisha yao
- Kuwa na mahusiano chanya baina ya wanawake na wanaume katika masuala ya maendeleo

2.8: Uwiano wa kijinsia

Tunaelewa nini kuhusu uwiano wa jinsia?

Uwiano wa kijinsia ni mkakati wa usawa wa kijinsia unaozingatia upatikanaji wa haki, fursa, mafao na nafasi sawa kwa wanawake na wanaume, watoto wa kike na watoto wa kiume bila upendeleo. Mfano; elimu ya msingi kwa wote Tanzania umefikia uwiano wa 50/50 kwa wasichana na wavulana.

Mkakati wa uwiano wa kijinsia unaangalia zaidi usawa katika ufikiaji wa huduma na mafao na unaozingatia mahitaji muhimu ya kijisni kwa mfano kuwapo kwa huduma bora ya afya ya uzazi inayojali utu wa mwanamke.

2.9: Uchambuzi wa kijinsia

Huu ni utaratibu mahsusi wa kuchambua, kuainisha na kuelezea kwa kina masuala ya kijinsia katika michakato ya maendeleo, ikiwepo mipango, bajeti na hata utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini ya maendeleo. “

Jinsia’ inatumika kama zana ya uchambuzi wa masuala mbalimbali, mfano, unapojenga shule, umezingatiaje kwamba kuna wengine wanatoka mbali hivyo wanahitaji kukaa katika mabweni, je, umezingatia vipi mahitaji ya watu wenye ulemavu? Uchambuzi wa jinsia unachambua mapengo ya jinsia katika fursa, haki, mafao na hata kudhihirisha wapi kwenye, ubaguzi, ukandamizaji na unyanyasaji

.Uchambuzi wa jinsia unasaidia kuandaa vigezo na viashiria vya kufuatilia na kutathimini matokeo ya mchakato au mpango wa maendeleo kwa wanawake na wanaume na watu wenye ulemavu.

Mfano wa uchambuzi wa ushiriki wa wanawake katika uongozi:

Uchambuzi wa jinsia utaonyesha ni nani yupo wapi katika nafasi za maamuzi na siasa, wanawake na wanaume wanashiriki kwa kiasi gani katika mchakato wa uchaguzi.

Ni muhimu kuwa na nyenzo za kuongoza uchambuzi wa jinsia

Mikakati maalumu ya kuwezesha wanawake (Affirmative Action)

Ni nafasi maalum zinazotolewa kwa wanawake au makundi ya kijamii yaliyoachwa pembezoni na si mikakati ya upendeleo kama mitazamo mingi ya kijammi inavyoonyesha. kwa mfano wanawake kushiriki katika maamuzi kwa kupewa nafasi ya kuchaguliwa katika uongozi kupitia viti maalum vya wanawake bungeni au udiwani. Huu ni mpango mkakati maalum wa kuziba mapengo ya jinsia yaliyoletwa na kutokuwepo usawa wa kijinsia katika maendeleo. Mkakati huu hutakiwa kwenda sambamba ni ule wa kuandaa wanawake waweze kuingia katika mifumo mikuu ya maendeleo ikiwemo ya maamuzi.

2.10: Sera pofu kijinsia

Hii ni sera ambayo inaelekeza maendeleo kiujumla bila kujali mahitaji na matakwa tofauti ya wanawake, wanaume, vijana na makundi ya kijamii yaliyowekwa pembezoni. Sera za aina hii hunufaisha zaidi wale walio kwenye mifumo mikuu.

Sababu kuu za kuwepo sera pofu ni kuwa na misimamo hasi na uelewa hafifu kwa watengeneza sera wengi wao wakiwa wanaume; mchakato wa sera kutokuwa shirikishi, na wengi wa watengeneza sera kutokuwa na ujuzi wa kuandaa sera zenye mtazamo wa jinsia.

2.11. Ni nini madhara ya ukatili wa jinsia

Ukatili wa kijinsia una athari nyingi kwa wanawake zikiwamo kuumizwa kimwili, kisaikolojia na kukosewa haki ya utu. Athari hizi zinaonekana zaidi kwa wanawake na watoto wa kike. Upo umuhimu kwa viongozi kutambua uhusiano uliopo kati ya ukatili wa kijinsia na umaskini wa wanawake.

2.12: Ukombozi wa mwanamke kimapinduzi

Ni nini vidokezo vya msingi vya dhana hii?

Huu ni mkakati mahsusi na mpana unaojikita kwenye kubomoa mifumo kandamizi ukiwamo mfumo dume, kuhoji masuala ya matabaka na ya makundi ya watu/sehemu nyingine kuachwa pembezoni (ikiwepo kutokuwapo usawa kati ya sehemu za mijini na vijijini).

Ili mkakati huu ufanikiwe kuleta ukombozi wa kimapinduzi kwa mwanamke na makundi yaliyo pembezoni ni sharti kuwepo ujenzi wa nguvu za pamoja ili kuunganisha nguvu na sauti dhidi ya mfumo kandamizi/mdumo dume.

2.12.1: Nini athari za upofu wa sera kijinsia?

Upofu wa sera kijinsia unaweza kuwa na madhara katika kuteua wawakilishi kama misingi ya usawa wa kijinsia hautafuatwa, au kuteua sehemu za kuweka huduma ya maji au sehemu ya kujenga shule, kama umbali kutoka makazi hautazingatiwa ipasavyo ni wazi kuwa malengo halisi ya maendeleo hayatafikiwa.

2.13. Ukatili wa kijinsia

Ukatili wa kijinsia ni kitendo cha ukatili anachofanyiwa mtu kwa msingi wa kijinsia ambacho husababisha madhara Kitendo kama hicho huhesabiwa kama uvunjifu wa msingi wa haki za binadamu zikiwamo haki ya kuishi, uhuru, usalama, utu, haki ya kuwa na hadhi kimwili na kiakili, haki ya usawa kati ya mwanamke na mwanamme, haki ya kutobaguliwa, haki ya kusikilizwa na kuheshimiwa mawazo.

2.13.1: Ni aina zipi za ukatili wa jinsia zimeripotiwa Zanzibar?

Tafiti mbalimbali zimeonyesha kuwepo ubakaji, ukiwamo ubakaji ndani ya ndoa, rushwa ya ngono, kuwapiga wanawake, mimba za umri mdogo, ndoa za kulazimishwa, biashara ya binadamu (kupeleka wasichana kufanya kazi nje ya nchi kwa ujira mdogo na manyanyaso makubwa), wanawake kutelekezwa na waume na wenzi wao na kuachiwa watoto, kuwabagua watu wenye ulemavu, wanawake kutopewa haki ya kumiliki ardhi. Hizi ni baadhi tu kwani suala la ukatili wa kijinsia bado limezungukwa na ukimya mkubwa.

2. 14: Uwezeshaji wa wanawake

Ni mchakato na pia mkakati unaowawezesha wanawake na wasichana kutambua mifumo na mazingira ya ubaguzi, uonevu na ukandamizaji inayowazunguka na kuhamasisha juu athari zake kwa maisha yao na haki zao za binadamu. Hamasa hii huwapelekea wanawake kuamua kuchukua hatua madhubuti za kubomoa mifumo kandamiza na kuleta mabadiliko.

Uwezeshaji wa wanawake ni muhimu kwa vile wanawake wameachwa nyuma kisiasa kwa miaka mingi na pia hakuna jitihada Madhubuti zinazochukuliwa na wadau wote kuwakwamua kutoka dimbwi hilo.

2.15: Nini kifanyike ili kufanikisha mabadiliko?

- ❖ Kujenga ujuzi na stadi za wanawake ili kuibua na kuchambua sababu zinazopelekea wao kuwa na hali duni.
- ❖ Kubadilisha fikra mgando kwa wao wenyewe na kwa jamii nzima kuhusu wanawake
- ❖ Wanawake na wasichana kujiamini na kujithamini na kuchukua nafasi za uongozi katika kila ngazi.
- ❖ Wanawake kushiriki shughuli za harakati za ukombozi wa mwanamke kimapinduzi zitakazopelekea kuleta mapinduzi ya kijamii, usawa wa jinsia na kukuza uwezo wa wanawake.

Kukuza uwezo wa wanawake kwa;

- ➢ Kuwa na ustawi na kufikia mahitaji ya kawaida na huduma muhimu za jamii.
- ➢ Kufikia na kutumia na kumuliki rasilimali, maarifa na teknolojia.
- ➢ Kuhamasika na kuingia katika harakati za kuleta mabadiliko na kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha sauti zao zinasikika
- ➢ Kuchukua nafasi katika mifumo ya maamuzi na uongozi

2.16: Uongozi Shirikishi, Jinsia na Demokrasia

Demokrasia ni mfumo unaofanikisha utawala wa watu kwa manufaa ya watu wa jinsia, rangi na rika zote. Kwa ufanisi halisi mfumo huu, sharti ujikite katika misingi ya usawa kijinsia kwani wanawake na wanaume huwa na mtazamo tofauti katika kushughulikia masuala yao ya kijamii na maendeleo. Ni dhahiri kwamba mahitaji ya wanawake katika nyanja ya afya, elimu na uchumi yatapambanuliwa kwa makini zaidi na wanawake kulingana na faida na athari wanazokabiliana nazo.

Mila na desturi ndani ya jamii yetu, zimejenga mfumo dume unao mwezesha mwanaume kupata fursa za maendeleo, kumiliki rasilimali na kuwa katika uongozi na nyanja za kutoa maamuzi kuliko ilivyo kwa mwanamke. Masuala ambayo yanakinzana na demokrasia.

> Demokrasia ni dhana katika mchakato wa siasa za nchi, ambapo raia wote wana haki sawa kushiriki. Ikimaanisha kwamba wanaume na wanawake na vijana wana nafasi na fursa sawa kutumia haki yao ambayo ni ya Kikatiba.

Uwiano kijinsia katika siasa na nafasi za maamuzi ni kiashiria cha Demokrasia iliyosimamia maadili ya haki na ushiriki wa wanawake na wanaume katika ngazi zote. Serikali inayojali zaidi ushiriki au maslahi ya jinsi moja zaidi, hiyo si ya kidemokrasia.

Demokrasia pia ni kipengele muhimu kwa maendeleo kijamii, uchumi na siasa za nchi. Demokrasia ni tupu iwapo watu wengi hawana uhakika wa chakula, elimu, matibabu, maji safi, njia za usafiri,

masoko nk. Mahitaji ya msingi katika maisha yanawezekana pale penye demokrasia ya kweli na ambapo wananchi, wanawake kwa wanaume, vijana na watu wenye ulemavu wana uhuru, fursa na uwezo wa kumiliki rasilimali zao kwa manufaa yao.

2.17: Uongozi

2.17.1: Nini uongozi?

Ni mchakato ambao unamwezesha mtu kushajiisha jamii au kuonyesha njia ili jamii iweze kufikia malengo fulani waliyojipangia kwa maslahi yao yenyewe. Kuongoza ni kuwa mstari wa mbele kwa maaana ya kutoa mawazo kuonyesha mwenendo mwema na vitendo vizuri.

Takwimu zinaonyesha kuwa wanawake ni 51% ulimwenguni lakini bado uwakilishi wao ni mdogo sana katika vyombo vya maamuzi kuanzia ngazi ya chini hadi taifa.

2.17.2: Kiongozi ni nani?

Ni mtu au watu waliochaguliwa au kuteuliwa katika jamii, kikundi au jumuiya kuwaongoza wengine kwa lengo la kufikia malengo yaliyowekwa. Kiongozi ana jukumu la kuonyesha njia na wala siyo kuwa bwanyenye. Kiongozi bora ni yule anayesikiliza maoni ya anaowaongoza na kuyafanyia kazi. Kiongozi anapaswa awajibike kwa jamii iliyomchagua. Kiongozi anapaswa awe mtumishi wa wananchi.

2.17.3: Aina ya uongozi:

1. Uongozi wa kidemokrasia
   Huu hupatikana kwa njia ya ya kufanya uchaguzi ulio huru na wa haki ama kwa kuteuliwa.

2. Uongozi wa kidikteta
   Unapatikana kwa njia ya mabavu ambapo utashi wa kiongozi wa juu ndio unaotawala zaidi kuliko mawazo ya wengi.

2.17.4: Sifa za kiongozi

- ✓ Awe na umri kuanzia miaka 18 na mwenye akili timamu na ajue kusoma na kuandika.Awe ni mwanachama wa chama cha siasa na awe mwanachama hai.
- ✓ Aifahamu vizuri sheria ya uchaguzi, haki na wajibu wake kama mgombea.
- ✓ Awe tayari kutafuta watu wa kufanyakazi pamoja hasa katika harakati za uchaguzi
- ✓ Awe mwaminifu na mwenye kujiamini na mwenye kuwajibika katika jamii.
- ✓ Awe na moyo wa uvumilivu, asiwe na dharau na aweze kukabiliana na changamoto mbalimbali.

- ✓ Awe muwazi, mwenye kujitolea na mfuatiliaji wa matukio na kupata habari zinazohusu jamii na nchi nzima.

- ✓ Awe ana mtizamo wa kijinsia na kutetea usawa na aweze kuchambua masuala yanayohusu wanawake.

- ✓ Awe mpenda watu na asiwe mbaguzi, aheshimu mawazo ya wenzake, akubali kukosolewa na kukubali mawazo ya wenzake.

2.18: Nini hali ya ushiriki wa wanawake katika uongozi wa siasa?

Viongozi wa siasa huchaguliwa kupitia mchakato wa demokrasia ambapo wananchi hushawishiwa kuchagua kiongozi bora na anayewajali, kuheshimu na kuwathamini watu wake.

Katika michakato ya uchaguzi wa viongozi wa siasa wanawake wapigakura huwa wengi kuliko wanaume kwa hiyo kiongozi anachaguliwa kwa kura sharti ashirikishe jinsi zote katika maamuzi, Hata hivyo ongezeko la uwakilishi wa wanawake kutoka majimbo ya uchaguzi umekuwa ukiongezeka kwa kasi ndogo mno ukilingalinisha na idadi ya wanawake katika nchi yetu ambao ni takribani ni asilimia 51.

2.19.1: Je, mwanamke anaweza kuwa kiongozi bora?

Tafiti zinaonyesha kuwa wanawake wanafanya vizuri katika nafasi za uongozi kutokana na kwamba ni watu wa kutimiza ahadi, ni watu wa kujitolea, si wapenda rushwa, wana heshimu usawa, jinsia na ni waadilifu.

Wanawake wameleta mafanikio mengi makubwa duniani. Kwa mfano:

Bibi Ellen Johson Sirleaf amekuwa rais wa kwanza mwanamke barani Afrika baada ya kushinda katika uchaguzi wa mwaka 2005 na ameshika wadhifa huo hadi mwaka 2017. Anasifiwa kwa kuirejeshea amani Liberia akiwa ni Rais wa 24 wa nchi hiyo.

Hata hivyo yeye sio mwanamke wa kwanza kuongoza nchi barani Afrika. Malikia Zauditu wa Ethiopia aliongoza nchi yake kwa miaka 13 toka mwaka 1917 hadi 1930. Mwanamke mwengine aliyepewa nafasi ya kuongoza nchi ni Bibi Sahle-Work Zewde wa Ethiopia ambaye Oktoba 2018 Bunge la Ethiopia lilimteua kuwa Rais wa nchi hiyo na ameweza kuleta mabadiliko makubwa ya kiutawala kwa muda mfupi tokea kuchaguliwa. Rais Ameena Gurib wa Mauritius amepelekea nchi hiyo kuendelea kuongoza katika Utawala bora Afrika chini ya Kipimo cha Mo Ibrahim, 2018. Bi Amina mahususi alianzisha msingi wa Mawaziri kufuata utaratibu wa utumishi wa kutokusimama katika upande wowote wa chama cha siasa na kuhakikisha kuwa hakuna mgongano wa kimaslahi baina ya majukumu yao ya kazi na maisha yao binafsi.

Mwezeshaji awape kazi washiriki ya kuainisha viongozi wanawake katika Bara la Afrika ambao ni mfano wa mabadiliko.

2.20: Nini hali ya ushiriki wa wanawake katika uongozi wa siasa?

Viongozi wa siasa huchaguliwa kupitia mchakato wa demokrasia ambapo wananchi hushawishiwa kuchagua kiongozi bora na anayewajali, kuheshimu na kuwathamini watu wake.

Katika michakato ya uchaguzi wa viongozi wa siasa wanawake wapigakura huwa wengi kuliko wanaume kwa hiyo kiongozi anachaguliwa kwa kura sharti ashirikishe jinsi zote katika maamuzi, Hata hivyo ongezeko la uwakilishi wa wanawake kutoka majimbo ya uchaguzi umekuwa ukiongezeka kwa kasi ndogo mno ukilingalinisha na idadi ya wanawake waliopo nchini.

2.21: Tunatarajia nini kwa viongozi wanawake katika nafasi za maamuzi?

Viongozi wanawake katika nafasi zao watoe msukumo kwa uwezeshwaji wa wanawake, wasichana, wanawake wenye ulemavu na usawa wa jinsia;

- Waongoze kwa misingi ya demokrasia shirikishi na haki za binadamu
- Walinde na kuhakikisha ralisimali zinapatikana kutekeleza haki za wanawake zilizoainishwa katika Katiba
- Kubuni michakato ya makusudi ili kuwezesha usawa kijinsia katika nyanja zote
- Walinde rasilimali ya Taifa isiporwe bali itoe msukumo kwa mipango na michakato itakayoelekeza rasilimali za taifa katika kujenga jamii yenye ustawi na usawa wa jinsia.
- Kuwa ni chachu kwa vijana wa kike kupata moyo wa kujituma ili kufikia uongozi wa hali ya juu
- Kusaidia nchi kufikia utawala bora kwa vile wanawake ni zaidi ya asilimia 50 ya watu wote hivyo kama hawamo kwenye uongozi ni kwamba kundi kubwa la jamii litakuwa halifaidiki na rasilimali za nchi.

2.22: Uongozi shirikishi

Uwiano wa karibu wa uongozi ulio sawa kati ya wanaume na wanawake ni lazima. Uongozi shirikishi ni utawala wa kidemokrasia uliojengwa kwenye misingi wa ushirikishaji wa watu katika maendeleo yao na fursa sawa kijinsia.

Uongozi shirikishi pia husimamia misingi ya demokrasia inayoongoza kwa kuweka watu na maendeleo yao mbele. Kiongozi anayeongoza kwa misingi ya demokrasia huwasikiliza wananchi wake na kutekeleza matakwa na mahitaji ya jamii husika bila ya ubaguzi, ukiwemo ule wa kijinsia.

Malengo ya mafunzo ya sura ya 2

- **Kuelewa mifumo ya kimataifa na kitaifa juu ya haki ya wanawake kushiriki katika siasa**
- **Kufahamu fursa zilizoainishwa kwenye mifumo ya kimataifa na kitaifa**
- **Kufahamu changamoto za kushiriki kaika siasa na uongozi.**

Moduli ya 2
Haki ya Wanawake Kushiriki katika Siasa

1.0: Utangulizi

1.1: Nafasi ya mwanamke katika kupigania uhuru

Mapinduzi ya Zanzibar

Wanawale walishiriki kikamilifu katika Mapinduzi ya Januari 12, 1964 yaliyotokea Zanzibar. Mfano Bi. Pili Jaha Ubwa wa ASP alikuwa ni mwandika hotuba mahiri, alikuwa akiwaandikia viongozi wanasiasa hotuba zao wakati wa kupigania uhuru. Alipata mafunzo ya kutayarisha hotuba nchini Ghana pamoja na Bi. Mwajuma Koja, Mwanaasa Khamis na Atiya Bushir. Hao walikuwa ni baadhi ya wanaharakati wanawake kwa Zanzibar wa zama hizo (Fair, 1994, 112)

Tukiangalia mfano wa Chama cha TANU, wanawake walikuwa mstari wa mbele katika kupigania uhuru (Geiger, 1997, p.57). walijitolea maisha yao wakati walipokuwa wakiandaa mikutano na kutafuta wanachama wa kujiunga na TANU wakati huo wanaume wakifanya siasa za chini kwa chini kwa kuhofia kukamatwa, kufungwa na kupoteza kazi.

Hali kama hiyo pia ilitokea Zanzibar ambako wanawake walikuwa ndiyo nguvu na tegemeo kubwa la mapambano ya ukombozi. Mwaka 1929 wakati wananchi walipopinga kodi ya ardhi na nyumba, wanawake walikuwa robo tatu ya watu waliojitokeza kupinga kulipa kodi ya ardhi na nyumba. Waliandamana kutoka mjini hadi Kibweni nje kidogo ya mji wa Zanzibar ambako ndiko ilipokuwapo nyumba ya Sultan na huko walikumbana na vitisho na vipigo vya polisi (Fair, 1994, p.128). Wakati polisi walipoamua kutumia njia ya makubaliano, washiriki wa mgomo huo wanaume walikubali kuingia ndani ya gari za polisi ili warudishwe mjini wakafanye mazungumzo ila wanawake hawakukubali hadi walipopata fursa ya kukutana na Sultani. Wanawake walikuwa wakiwahamasisha watu nyumba kwa nyumba ili wahudhurie mikutano ya hadhara, walikuwa wakitoa ujumbe kupitia nyimbo walizozitunga, mashairi na hata kupitia kwenye khanga. Kadhalika walijitolea mali zao kama vile nyumba na ardhi kwa ajili ya kuchangaia harakati za vyama vya siasa. Pia walitengeneza kadi za chama, khanga na chakula walivyoviuza ili kupata michango zaidi. Pamoja na jitihada zote mchango wa wanawake haukuelezwa katika historia ya kudai Uhuru/Mapinduzi.

1.2: Haki ya ushiriki wa siasa

Haki ya ushiriki wa siasa inatambulika kimataifa, ikiwa pamoja na uhuru wa kujumuika, uhuru wa kujiunga katika jumuiya na haki ya kufaya shughuli za serikali na hakutakuwa na ubaguzi wowote kwani katiba ya Zanzibar sura ya tatu kifungu 11(1) imeeleza Binadamu wote huzaliwa huru na wote ni sawa ingawa haikuelezwa moja kwa moja, na kueleza katika kifungu 21(1) kuwa kila mzanzibari ana haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa wanchi ama moja kwa moja au kwa kupitia uwakilishi waliochaguliwa kwa hiari au lakini katiba ya Zanzibar kifungu 20 (1) Imeeleza kuwa kila mtanzania ana haki kwa amani na usalama kujumuika na kuwa na maingiliano na wenziwe kuweza kueleza mawazo/maoni yake na kujiunga na au vyama vya siasa kwa utashi wake. Katika katiba hiyo ya Zanzibar kifungu namba 7 (1)(2) kimetambua haki ya kupiga kura au kugombea katika uchaguzi na kushiriki katika shughuli za utawala.

Tanzania imeridhia mikataba mbali mbali ya kimataifa na kikanda ambayo inasisitiza haki za wanawake za kushiriki na kutaka serikali zilizoridhia mikataba hiyo kuweka mikakati ya kuhakikisha ushiriki wa wanawake katika kuongoza, na haki ya kutobaguliwa kwa vigezo vya jinsi au jinsia. Baadhi ya Mikataba hii ni pamoja na: Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza aina zote za ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW), Mkataba wa Nyongeza wa Jinsia na Maendeleo, ya Shirika la Maendeleo la Kusini Mwa Afrika, Mkataba wa nchi Huru za Kiafrika kuhusu haki za binadamu.

Kwa muda mrefu madhila na manyanyaso ya wanawake katika jamii za Tanzania yalikuwa hayaripotiwi kwa sababu jamii ilikuwa ikiona kuwa matendo anayofanyiwa mwanamke ni ya kawaida sana na ndiyo mwenendo wa jamii husika, hivyo kupigwa, kubakwa na hata kutoshirikishwa katika maamuzi hata yalke yanayomuhusu yeye mwenyewe ndivyo utamaduni ulivyokuwa ukielekeza. Hivyo mwanamke ni mtu wa kuamuliwa na kutendewa tu, ni mtu wa kuongozwa na kupangiwa bila kuzingatia hisia zake, mapenzi yake na matakwa yake kama binadamu.

2.0: Mifumo ya kimataifa na ushiriki wa wanawake katika siasa na uongozi

2.1: CEDAW

Huu ni mkataba wa kimataifa unaopinga aina zote za udhalilishaji, mkataba huu umeasisiwa mwaka 1979 na umeweka vipengele/vifungu mbali mbali vinaonyesha kukata za na kupinga aina zote za udhalilishaji na ubaguzi kwa wanawake ikiwa pamoja na kumbagua mwanamke kutoshiriki katika siasa na uongozi . Katika mkataba huu kifungu cha 7 kimeelza wazi kuhusu ushiriki wanawake katika shughuli za siasa na maisha ya kijamii. Pia mkataba umeendelea kusema kuwa haki sawa baina ya mwanamke na mwanmme katika uchaguzi na mchakato mzima wa upigaji kura pamoja na kuchaguliwa kushika madaraka. CEDAW ni mkombozi wa wanawake katika uwanja wa siasa na kuwashajihisha kupiga kura na kupigiwa kura bila ya kubughudha au unyanyasaji wa kijinsia.

2.2: Itifaki ya Maputo

Haya ni makubaliano yaliofanyika tarehe 11, Julai, 2003 nchini Msumbiji katika mji wa Maputo, katika kipengele namba 9 cha makubaliano haya imeonesha haki ya kushiriki wanawake katika siasa na katika mchakato wa kushiriki katika vyombo vya kutoa maamuzi. Makubaliano haya yametoa fursa mbali mbali kwa mwanamke kugombea nafasi za uongozi na nchi kwa kuweka mazingira mazuri ya kumweza wanawake kupata fursa hizo.

2.3: Jukwaa la utendaji kazi la Beijing

Mpango wa utekelezaji wa Beijing katika maelezo ya dhamira namba 7 ya mpango huo imeeleza kuhusu uwezeshaji wa wanawake na ushiriki katika vyombo vya maamuzi kwa kuangalia upogo katika uwiano wa kijisia (nafasi walizonazo wanaume na wanawake katika ngazi za maamuzi) ili kuhakikisha kuwa wanawake na wanaume wanapata nafasi sawa ya kushiriki katika ngazi zote za uongozi.

2.4: Itifaki ya SADC

SADC ni Jumuiya ya maendelo ya nchi za Kusini mwa Afrika na SADC Protocol ni mkataba wa kikanda wa nchi za kusini mwa Afrika uliotiwa saini 2008 wenye vifungu 43 ambavyo vinaelezea kuondoa utafauti na kuwatenga wanawake katika nyanja mbali mbali za maendeleo na kuwasaidia kupata usawa wa kijinsia nchini mwao. Kifungu namba 12 na kifungu namba 13 vinahusika na maendeleo ya wanawake kisiasa.

Kifungu namba 12 kinasisitiza ushiriki sawa wanwake kufikia asilimia 50/50 kwenye njanja ya za maamuzi serikalini na taasis binafsi. Pia juhudi zifanyike kupatiwa mafunzo na kampeni kuelimisha jamii umuhimu wa ushiriki na uwakilishi sawa bina ya wanwake na wanume kwenye nafasi za maamuzi kulinda demokrasia na utawala bora. Kifungu namba 13 cha mkataba huu kinaelezea kuwekwe mikakati madhubuti kuwawawezesha wanwake kushiriki katika michakato mizima wa uchaguzi na upigaji kura. Pia wanawake wawezeshwe kwa njia za mafunzo na kushajihishwa kushiriki katika nyanja za siasa na kuondosha mila na desturi potofu zinazopingana na maendeleo ya mwanamke katika siasa na uongozi

2.5: Mifumo ya kitaifa na ushiriki wa wanawake katika siasa na uongozi

Mifumo ya kitaifa iliyoeleza haki ya wanawake kushiriki katika ulingo wa siasa na uongozi ni pamoja na Katiba ya Zanzibar, Dira ya Zanzibar ya 2020, Mkakati wa kupunguza umasikini na kukuza uchumi, Sera ya jinsia ya Zanzibar, sheria ya vyama vya siasa na sheria ya uchaguzi ya Zanzibar.

> Mwezeshaji atafundisha mada hii kwa kuelezea mfumo mmoja mmoja na kutoa mifano na kuwataka washiriki waelezee hali halisi ikoje licha ya mifumo ya nchi inavyoeleza wazi juu ya ushiriki wanawake katika ulingo wa siasa na uongozi.

2.6: Katiba ya Zanzibar ya 1984

Katika kifungu 21(2) Kila Mzanzibari anayohaki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomuhusu yake na yanayohusu Taifa lake.

Katiba ya Zanzbar 1984, marekebisho ya 2010 imeeleza wazi katika kifungu namba 67(1) kuwa kutakuwa na wajumbe wa Baraza La Wawakilishi wanawake kwa idadi ya asilimia arubaini (40%) ya wajumbe wote wa kuchaguliwa katika majimbo

2.7: Sera ya Jinsia na Ushirikishwaji wa jamii ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC)

Katika kuhakikisha kuwa wanawake na makundi ya walio pembezoni haki zao zinazingatiwa katika michakato ya demokrasia na uchaguzi, mwaka 2015 ZEC ilitengeneza sera ya jinsia ambayo lengo lake ni kuhakikisha ushiriki na uwakilishi ulio sawa wa raia wote. ZEC imeweka mikakati na hatua za kuchukuliwa kuhakikisha uwepo wa usawa wa jinsia na ushiriki wa makundi yote yaliyo pembezoni wakiwa kama wapiga kura na wagombea. ZEC itahakikisha kuwa mahitaji maalum ya wanawake na makundi yaliyo pembezoni yanathaminiwa na kufuatiliwa kwa karibu kila mara na hatua madhubuti zinachukuliwa kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika demokrasia na uchaguzi.

2.8: Dira ya 2020

Dira ya Zanzibar lengo namba 5 limeeleza kuwa kuhusu kuwaendeleza wanawake kwa kuinua na kutoa nafasi za uongozi kwa wanawake katika jamii na kuongeza fursa na kuwa wenza katika vyombo vya utoaji wa maamuzi katika shughuli za uchumi, kijamii na kisiasa katika ngazi zote za utawala.

2.9: Sera ya Jinsia ya Zanzibar

Katika Sera ya Jinsia sura ya nne imeonesha katika suala la sera kuwa namba 4.1 kuwa ushiriki wawanawake katika vyombo vya utoaji maamuzi katika ngazi zote ni mdogo. Hivyo serikali kwa kushirikiana na wadau wengine watachukuwa juhudi za makusudi kuona ushiriki na ushirikishwaji wa makundi yote; wanawake na wanaume katika ngazi za maamuzi

Mikakati ya kisera itafanyika ikiwa ni pamoja na:

- ✓ Kushawishi katika kuongeza asilimia 50% ya wanawake katika nafasi za uongozi katika ngazi zote pamoja na wanwake kuwemo katika baraza la wawakilishi ikiwa serikali kuitikia wito wa makubaliano ya utelezaji wa SADC Protocal.
- ✓ Kuhamasisha vyama vya siasa kuteua wanawake kugombea katika chaguzi
- ✓ Kuhamasisha kufanyiwa mapitio katiba za vyama siasa ili kuweka vigezo vya uteuzi wa wagombea ikiwemo viti maalum vya wanawake.
- ✓ Kuinua usawa wa kijinsia kwa kufanya juhudi za makusudi za kuongeza idadi ya wanawake katika nafasi za uongozi katika sekta za umma na za binafsi.

2.10: Uislam unasemaje kuhusu wanawake kuingia katika uongozi?

Baadhi ya Waislamu wanadai kuwa mwanamke hafai kuwa na nafasi za uongozi wa kifamilia seuze kitaifa kwani pahala pake ni nyumbani ili alee watoto. Wengine wamediriki kusema na kutamka bila elimu sahihi kuwa mwanamke kufanya kazi ya uongozi ni haramu kwani Aya ya Qur-ani imeshasema kuwaambia wanawake kuwa ((*Na tulieni (enyi wanawake) majumbani mwenu*)). Ahzab 33

Wanachuoni wameijibu hoja yao hiyo kama ifuatavyo:

a- Aya hii inawahusu wake za Mtume tu ambao wana hukmu yao peke yao katika jambo hili na baadhi ya mambo mengine. (Dr. Qardhawy)

b- Mama Aisha alitoka nyumbani kwake na kushuhudia vita vya ngamia kwa vile amehisi kuwa ana wajibu wa kidini wa kusaidia kuondosha uovu kutokana na kuwa ni muislamu bali kwa nafasi yake ya uongozi kwa kuwa aliwahi kuwa "first lady".

c- Wanawake wametoka na kufanya kazi (daktari, walimu n.k) bila ya kutokea madhara yoyote kwake na kwa jamii. Aidha tumeuona mchango wa wanawake tuliokwisha wataja hapo juu ambao pengine kama si mchango huo na wa wanawake wengine Uislamu usingetufikia leo hii hapa tulipo.

Pia wengine wanatumia aya ya suratun nisaa (34) kutafsiri visivyo kuwa *wanaume ni viongozi wa wanawake wakati tafsiri sahihi ni "Wanaume ni wasimamizi wa wanawake".*

Jibu la hoja hiyo lililotolewa na Maulamaa ni kuwa, Aya inayozungumzia hali hiyo ya "*qawamah*" imeashiria vyema kwamba hali hiyo ni katika maisha ya ndani ya familia ambapo kila mmoja kati ya mke na mume kapangiwa majukumu yake maalumu ambayo yanakubaliana na maumbile yake. Kwa hivyo mwanamume anatakiwa abebe jukumu zito zaidi la kutoa mali yake kwa kuhudumia familia nzima ambapo mwanamke kimaumbile ana jukumu la kubeba ujauzito na kujifungua.

Kuna wanawake masahaba ambao ni mashuhuri kuwa walitowa michango mikubwa katika nyanja mbalimbali zikiwemo za uongozi, utawala na utumishi wa Umma hadi Uislamu ukasimama. Mfano wa hao ni hawa wafuatao:

a) **Bi Raqiqah bint Safiyy**: Huyu ndiye aliyegundua njama za Makuraish za kutaka kumuuwa Mtume au kumfukuza katika mji wa Makka. Licha ya kuwa umri wake ulikaribia miaka 100 moja, haukumzuwia kutumia nafasi yake ya kuyalinda maisha ya Mtume SAW. Tukio hilo lilikuwa ni katika sababu zilizopelekea Hijra ya Mtume kwenda Madina.

b) **Bi Asmaa bint Abi Bakar**: Nafasi yake ilikuwa ni utoaji wa taarifa na habari kwa Mtume SAW. Makuraish walipomshakia na kazi hiyo ya Wizara ya Habari kwa Uislamu alikanusha na alipata adhabu na manyanyaso makubwa kutoka kwa Abu Jahli. Lakini hakuwacha kuitekeleza nafasi yake.

c) **Nasibah bint Ka'ab**. Ni mwanajeshi wa mwanzo mwanamke katika Uislamu. Amepigana vita vya Uhud pamoja na wanaume ambapo alijeruhiwa mara 11 katika mwili wake wakati alipokuwa akimkinga Mtume asifikiwe na silaha za maadui wa Uislamu. Vita vyengine alivyopigana ni vya A'qabah, Hudaybiyah, Hunayn na Yamamah ambapo alipoteza mkono wake mmoja.

Kwa hivyo wanawake wana haki ya kuwa viongozi katika nyanja mbalimbali za kijamii.

((....Na saidianeni/shirikianeni katika wema na ucha Mungu, wala msishirikiane katika dhambi na uadui...)) – Al Maidah Aya 2. Uislam unahimiza juu ya haki ya kusaidiana kimawazo na kushauriana kwa kushirikisha wanawake na wanaume katika maswali mbali mbali ya kimaendeleo.

2.11: Je, ni changamoto gani anazozipata mwanamke anapotafuta nafasi ya uongozi?

a) Tamaduni na mifumo iliyojengeka ya kijamii haijawa tayari kuwaandaa wanawake kuingia katika uongozi/uchaguzi.

b) Ukosefu wa fedha za kuendesha kampeni na kutumia vyombo vya habari na kukosa wadhamini na wapambe hasa wakati wa kampeni.

c) Sheria dhaifu za uchaguzi na udhibiti mdogo wa rushwa.

d) Ukosefu wa elimu ya uongozi kwa ajili ya kufanya kampeni za kisiasa na kujieleza hadharani.

e) Mfumo dume uliojengeka katika vyama vya siasa ambapo uanachama na umuhimu wa wanawake huonekana kwa kuwapigia kampeni wagombea walio wengi ambao ni wanaume.

f) Utekelezaji mdogo wa mikataba mbali mbali ambayo serikali imeridhia CEDAW, BEIJING, SADC na ushirikishwaji mdogo wa wanawake katika masuala yote ya maendeleo pamoja na utekelezwaji wa mipango ya MKUZA.

g) Mfumo dume uliopo katika jamii ambapo huamini mwanamke hana uwezo wa kuwa kiongozi na kuweza kuleta mabadiliko ya kimaendeleo.

h) Wanawake wengi kutokujiamini kutokana na jinsi mfumo dume ulivyowakuza na kuwadumaza.

i) Wivu miongoni mwa wanawake wenyewe na kutokuungana mkono. Mara nyingine wanawake hurudishana nyuma.

j) Wanaume wanadhani kuwa wanawake wanahitaji kuonekana tu na siyo kusikika.

k) Wanaume kutokuwaunga mkono wanawake kujitokeza kugombea uongozi

l) Vyama vya siasa kutokuunga mkono kwa wanawake kwa ujumla na hasa kwa wanawake wanaostahiki. Badala yake hupendelea kuwapa nafasi wagombea wanaotoka kwenye familia mashuhuri. Utaratibu huo hunyima wanawake fursa ya kushiriki kugombea kwa sababu wengi wao hutoka kwenye familia masikini, hivyo hawapewi nafasi hata kama wanao uwezo wa kuwa viongozi.

m) Ndugu na jamaa kuwa na matarajio makubwa kuwa shida zao zitamalizwa na mgombea.

n) Wagombea wanawake huchunguzwa au kukejeliwa na wanajamii kuliko wenzao wanaume.

o) Wazazi, jamaa au waume wa wagombea wanawake huwa hawakubali binti au mke kugombea nafasi ya kisiasa kwa kuhofu hatari zilizomo katika siasa ndani zilizomo ya vyama

Malengo ya moduli ya 3

- Kuwawezesha washiriki kwa kuwapa ufahamu kuhusu umuhimu wa ushiriki wa wanawake katika uongozi
- Kuhamasisha jamii isaidie wanawake waingie kwenye ulingo wa siasa
- Kuelezea hatua kwa hatua namna itakavyoshiriki kuanzia ngazi ya wadi kuwasaidia wanawake kuingia katika ulingo wa siasa.

MODULI YA 3
Jamii na uongozi wa wanawake

1.0: Utangulizi

Jamii: Ni kikundi cha watu wenye kuwa na msimamo na mitizamo mimoja/tofauti, wanaishi katika aneo fulani na huzungumza lugha moja. Hivyo jamii inaweza kuwa eneo, familia katika kijiji ikiwa kila mmoja anamtegemea mwenzake kwa njia moja au nyengine katika maisha yao ya kila siku. Kwa upande wa siasa mara nyingi jamii inaonekana/kuwapo katika ngazi ya shehia, wadi au jimbo.

Uhamasishaji wa jamii: Ni mchakato unaoleta watu pamoja na rasilimali nyengine ili kufanya shughuli zitakazo sababisha kufikia malengo ya maendeleo endelevu. Maandeleo yanatakiwa kupangwa pamoja, kutekelezwa na kutathminiwa na wanajamii wenyewe. Haya hufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi ili mikakati hiyo shirikishi iweze kuwa endelevu ili kufikia malengo. Kwa upande wa ushiriki wa wanawake katika ulingo wa siasa wana jamii wa ngazi ya chini wanatakiwa kusaidiwa kupanga na kutekeleza shughuli ambazo zitawasaidia wanawake kupata nafasi za uongozi katika ngazi ya wadi, jimbo na Taifa.

Mchakato huu unaingiza masuala ya uchambuzi wa hali ikoje; mathalan kuwapo kwa viongozi wachache wanawake na wanaume wakiwa wengi kuchukuwa nafasi za uongozi katika ngazi ya wadi, majimbo na Taifa, kufahamu mambo yaliyopelekea kuchangia kuwapo kwa hali hiyo na athari za kuwapo kwa hali hiyo. Mwisho wa uchambuzi wanajamii wachukue hatua kwa pamoja kuondosha tatizo na baadaye kufanya tathmini baada ya utekelezaji wa hatua zilizochukuliwa.

Uhamasishaji wa jamii ni mchakato wenye dhamira ya:

- Kuiwezesha jamii kuainisha vipaumbele vyao, rasilimali, mahitaji na kupata suluhisho kwa changamoto zao kwa kufanya jitihada za pamoja ili kuinua ushiriki wao, utawala bora, uwajibikaji na mabadiliko endelevu
- Kuwaleta watu pamoja katika kushauriana kwenye dhamira, kuongeza uwezo wa mjadiliano, kujengeana uwezo na kuchukua hatua pamoja kushughulikia matatizo yanayowathiri wanajamii;

- Kujenga uwezo wa wanajamii, mmoja mmoja, au jumuiya kupanga, kutekeleza na kutathmini shughuli kwa ushirikiano na endelevu ili kufikia makubaliano yaliyo mwafaka kuhusu lengo lao la maendeleo.

Shughuli 2.2: Kazi ya vikundi

- Katika vikundi, jadilini umuhimu wa kuiandaa jamii
- Elezea umuhimu wa kuiandaa jamii kuwaunga mkono wanawake katika siasa

Nukta muhimu kukumbuka

Uhamasishaji jamii ni mchakato wa:

- Kuishirikisha jamii kuainisha vipaumbele vyake, rasilimali mahitaji na suluhisho katika hali inayokuza ushiriki, utawala bora, uwajibikaji na mabadiliko chanya.
- Kuwakutanisha watu kuwa na muono wa pamoja, kuhamasisha majadiliano, uchambuzi pamoja na kuchukua hatua ya pamoja katika kumaliza matatizo
- Kuongeza uwezo wa jamii, mtu mmoja mmoja, kikundi au taasisi kupanga na kutekeleza shughuli za kuhamasisha jamii na kufanya tathmini kwa pamoja ili kufikia lengo walilokusudia.

3.0: Umuhimu wa kuishirikisha jamii

Jamii inaposhirikishwa husaidia:

1. Kuwapo kwa mijadala ya kuendelea kuhusu mambo mbalimbali yanayoihusu jamii husika;
2. Kukuza uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa kushirikiana katika kutatua changamoto;
3. Kukuza uwezo wa wanajamii katika kuchambua mambo yanayosababisha changamoto zilizopo katika jamii
4. Kukuza uwezo wa wanajamii wa kutafuta sukuhisho na kuchukua hatua katika kutatua changamoto zinazoikablili jamii
5. Kuongeza uwezo wa wanajamii katika kufanya tathmini ya mambo na kusonga mbele kutokana na mafunzo waliyoyapata katika utatuzi wa changamoto
6. Jamii kuwa na umiliki wa masuala yaliyomo katika jamii na kuwajibika
7. Kuwasaidia wanajamii kushiriki katika kutoa uamuzi juu ya jambo linalowahusu, kufanya tathmini na kubeba dhamana kwa mafanikio na mapungufu juu ya suala walilolifanyia kazi kwa pamoja.
8. Kuibua mbinu za kutatua matatizo yanayotokea mara kwa mara
9. Kurudisha taratibu za asili za ushirikiano katika jamii ambao ndio msingi wa maendeleo.

3.1: Njia za ushirikishaji jamii kuwaunga mkono wanawake katika uongozi

Mchoro ufuatao unaainisha njia za kufuata katika kuishirikisha jamii kuwaunga mkono wanawake katika kuwania nafasi za uongozi.



Shughuli 3.2: Kazi za vikundi

- Lisome jedwali lililopo hapo chini na elezea kwa undani hatua muhimu za kuishirikisha jamii
- Chukua au jimbo, fikiria vipi utaihamasisha jamii kuwaunga mkono wagombea wanawake.
- Katika kolamu ya tatu andika mikakati utakayoitumia ili kuingiza wanawake katika uongozi wa kisiasa
- Wasilisha mikakati ya kundi lako

3.3: Jedwali la jinsi ya kuishirikisha jamii kuwaunga mkono wagombea wanawake waingie katika nafasi za kisiasa:

HATUA	MAELEZO	Mkakati au hatua za kina kuhusu vipi utafikia kila hatua katika kuihamasisha jamii kuwaunga mkono wanawake katika uchaguzi
1	Andaa uhamasishaji (Anzisha timu ya uhamasishajiTrain community Mobilization teams • Tengeneza mpango wa uhamasishaji • Wasiliana na wanajamii • Kusanya taarifa Zaidi kuhusu mambo yaliyomo katika jamii m.f rasilimali na vikwazo	
2	landae jamii kufanya kazi • Hamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwaunga mkono wanawake kupata nafasi za uongozi katika siasa. • Hamasishaji ushiriki wa jamii • Hakikisha kwamba wale wanaoathirika na tatizo (m.f; wanawake) wanashiriki. • Igawe jamii katika makundi maalum kuhakikisha uwepo wa ushiriki katika majadiliano	
3	Ibua hoja na weka vipaumbele • Ibua hoja kuhusu kuwatenga wanawake katika uongozi wa kisiasa • Chambua taarifa ikiwa ni pamoja na kuainisha sababu/chanzo cha tatizo • Weka vipaumbele	
4	Kupanga pamoja • Wezesha kikao cha mipango cha jamii • Ainisha hatua inayopaswa kuchukuliwa kulishughulikia tatizo	

	• Amua nani atashiriki, nani ataongoza mchakato, rasilimali zitakazohitajika • Elezea vipi ufuatiliaji utafanyika,	
5	Fanyeni kazi kwa pamoja • Huongeza uwezo wa jamii kufanyia kazi mpango mkakati wake. • Hakikisha kwamba jamii inatekeleza ilichokipanga. • Fuatilia mchakato • Fahamu matatizo na yasuluhishe, shauri na tatua migogoro • Ratibu pamoja na wadau a wengine	
6	Fanyeni tathmini pamoja • Andaa tathmini shirikishi kuona kama jamii imefikia malengo yake • Chambua matokeo kujua kama jitihada zimeleta mabadiliko na ni jitihada gani nyingine zifanyike siku za baadaye. • Peleka mrejesho katika jamii • Weka taarifa vizuri na eleze mafunzo uliyoyapata na mapendekezo kwa ajili ya baadaye.	

Modeli hii inaeleza kwamba unapaswa kuanza na mchakato wa uhamasishaji jamii kwa kuainisha changamoto unazotaka kuzifanyia kazi. Katika muktadha huu ni changamoto ya kuwa na wanawake wachache katka nafasi za uongozi katika ngazi za wadi na jimbo ukilinganisha na wanaume. Hatua ya pili ni kuweka mkakati/mpango wa kufanya kazi na jamii. Baada ya hapo utaibua mambo yote muhimu ili kufahamu hasa kinachotendeka katika jamii. Kwa kuongezea utaangalia mila, desturi au imani zinazomkandamiza mwanamke na kumkosesha haki yake au nafasi ya kushiriki katika siasa akiwa kama kiongozi. Ukishaainisha masuala yote, hapo sasa unaweza kuweka vipaumbele, kuandaa mpango wa kuufanyia kazi. Wakati wa utekelezaji wa programu unapaswa ufuatilie kwa karibu na mwisho ufanye tathmini.

Shughuli 3.4: Kutatua tatizo

1) Mpe kila mshiriki karatasi na kalamu
2) Kila mshiriki aandike changamoto moja ambayo mwanamke inabidi apambane nayo ili kupata uongozi kati wadi, jimbo au taifa
3) Washiriki waandike swali kuhusu changamoto anayoipata mwanamke anapogombea uongozi kwa mfano; Je, unadhani rushwa ni kikwazo kwa mwanamke kugombea?
   - Wachache wayasome majibu yao ili yajadiliwe.

4.0: Mambo ambayo jamii inaweza kufanya kuwasaidia wanawake kushinda/kung'ara katika uchaguzi ngazi ya wadi, jimbo au Taifa.

Mambo yafuatayo jamii inaweza kuwasaidia wanawake kushinda katika ngazi ya wadi, jimbo au Taifa:

1) Masheha na viongozi wa jamii wawe mstari wa mbele katika kuhamasisha jamii wawapigie kura wanawake ili nao washiriki kikamilifu katika kufikia maendeleo endelevu.
2) Jamii kuainisha wanawake wenye uwezo na sifa za uongozi, washajiishaji na walio mstari wa mbele katika kuleta maendeleo; hao wawahamasishe kugombea na wawaunge mkono wakati wa uchaguzi ili washinde.
3) Kushawishi na kufanya utetezi viongozi wao kuondosha mila, desturi, na imani zinazozuia wanawake kuchukua nafasi za uongozi katika siasa
4) Jamii kuwasaidia wagombea wanawake katika kupata nafasi za uongozi katika ngazi za kamati za shehia au kamati za wadi ili kuandaa jukwa la wanawake kuafanya mazoezi kabla ya kusimama kugomba katika kipindi cha uchaguzi
5) Wanajamii wanaweza kuwashawishi wanawake wanaowaona wanao uwezo kuwakilisha katika jamii yao
   (shehia au wadi yao) hivyo wawatake kugombea licha ya kuwa wengi wao hawana na uwezo wa kifedha.
6) Wanawake wapo wengi katika ngazi ya jamii na ya Taifa, hivyo kinachohitajika ni kufanyiwa kampeni kuwapigia kura wanawake wenziwao.
7) Jamii inapaswa kuwasaidia wagombea wanawake kuainisha matatizo halisi yaliyopo katika jamii ambayo yanahitaji suluhisho za kimaendeleo.
8) Wanajamii wanaweza kutoa ushauri kuhusu mambo mbali mbali ambayo yanahitajika katika kipindi cha uchaguzi.
9) Wanahitaji kubadilisha mitazamo yao hasi juu ya wanawake na wafahamu fika kuwa wanawake ni binadamu wenye vipaji na uwezo sawa na wanaume.
10) Jamii kusaidia kupigia kampeni wanawake wakati wa uchaguzi.
11) Jamii kuwapigia kura wanawake kutokana na sera zao na utashi wao wa kuleta mabadiliko chanya.
12) Kufanya utetezi wa kuundwa kwa sheria ndogo ndogo katika jamii ambazo zinaunga mkono wanawake kugombea katika wadi na majimbo.

4.1: Mfano wa uhamasishaji jamii kwa ajili ya kukuza ushiriki wa wanawake katika siasa katika wadi au jimboni:

Hatua ya 1	Ainisha tatizo kubwa lililopo katika wadoi au jimbo
Hatua ya 2	Panga na chagua stratejia ya kusuluhisha tatizo (mfano; fanya warsha ya watu muhimu katika jamii kwa ajili ya kuwahamasisha kuhusu jambo hilo (ushiriki wa wanawake katika siasa)
Hatua ya 3	Ainisha watendaji wakuu au wadau (Mwenyekiti wa kijiji, Imam, mkuu wa kaya n.k.)
Hatua ya 4	Hamasisha watendaji wakuu na wadau kufanya majadiliano na kukubaliana kipi cha kufanya.
Hatua ya 5	Tekeleza shughuli zote kwa mwelekeo wa kupata utatuzi wa tatizo (wekeza katika uhamasishaji wa watu waliopatikana katika warsha na fanya shughuli zitakazokuwezesha kufuatilia utendaji wa watu uliowaainisha)
Hatua ya 6	Tathmini matokeo ya shughuli ulizozifanya kutatua tatizo
Hatua ya 7	Ongeza shughuli kulingana na matokeo uliyoyapata katika tathmini yako.

Modeli hii ya uhamasishaji huwafanya wadau/wanajamii wajihisi kwamba mradi ni wao na wanaumiliki kwa sababu wameshiriki katika kuliibua tatizo, kulipangia mikakati na kutekeleza mikakati waliyojiwekea na kulitatua tatizo.

5.0: Umuhimu wa kujiandikisha kupiga kura

Kitu muhimu kwa wanajamii ni kuhakikisha kuwa wanawapigia kura wanawake wakati wa uchaguzi. Lakini hilo litawezekana tu ikiwa watu watajiandikisha kupiga kura.

Shughuli 5.1: Majadiliano katika vikundi

- Ainisha na jadili sifa za mpiga kura
- Eklezea masharti ambayo yakikiukwa mtu anaweza kuondoshwa katika orodha ya daftari la wapigakura

5.2: Miiko ya uchaguzi

Katika kuendesha michakato ya kisiasa ni vyema ni vyema kubeba misingi mikuu ya demokrasia ikiwa pamoja na kuwepo haki ya kupiga kura kwa watu wote wenye haki ya kupiga kura, ufargha wa kweny karatasi ya kupigia kura, urahisi wa kufikika eneo la kupigia kura na mazingira mazuri

kwa wote (wanwake wajawazito , watu wenye ulemavu, wazee), haki ya kila mwananchi kuwa mgombea (mwanamke, kijana..) ilimradi ana sifa na vigezo vinavyomruhusu kugombea, wananchi kuwa huru kushiriki katika vyama vya siasa na katika uchaguzi ambako pia mazingira yanapaswa kuwa huru na rafiki kwa mpigakura, kuwepo na tume huru ya uchaguzi na kutokuwepo/au kutofanyiwa vitisho vya aina yoyote.

5.2: Kujiandikisha

Kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar No 4, 2018 kifungu Namba 44 (a - f) na kifungu cha 45 (a – g) vimetaja sifa za mgombea kuwa ni mtu yeyote aliyetimia umri wa miaka 21, Mzanzibari ana makazi ya kudumu ana haki ya kuchagua au kuchaguliwa hivyo kabla ya kupiga kura kila mtu anatakiwa kujiandikisha na kuingizwa katika daftari la wapiga kura ambalo hutayarishwa na Tume ya uchaguzi ya Zanzibar au Tume ya Taifa ya uchaguzi. Ili kuhakikisha wanawake wanajitokeza kugombea ni vyema kuwahimiza kujiandikisha ili kuweza kupiga kura au kupigiwa kura. Bila ya kujiandikisha kama mpiga kura atakuwa amepoteza haki ya msingi ya kumchagua anayemtaka kuwa kiongozi wake au kuchaguliwa kuwa kiongozi.

5.3: Utambulisho wa wapiga kura na upigaji kura

Utambulisho ni kadi maalum ambayo hutumika kwa jaili ya kupiga kura siku ya uchaguzi. Kadi ya kupiga kura ni utambulisho pekee unaotumika ambao ndio unaowasaidia watendaji wa uchaguzi kufahamu kama mtu huyo ni mpigaji kura halali wa uchaguzi. Hivyo kila aliyejiandikisha kupiga kura anatakiwa kutumia kadi yake kupiga kura siku ya kupiga kura. Ni marufuku kumpa mtu mwengine kuitumia.

5.4: Mikutano ya kampeni

Ni Mikutano inayoandaliwa na wagombea kupitia vyama vyao vya siasa kunadi sera na kutambulisha wagombea wao kwa wananchi ili waweze kuchaguliwa.

5.5: Kupiga kura

Ni kitendo kinachofanyika siku ile ya uchaguzi ambao watu wote wenye vitambulisho vya kupiga kura na wameorodheshwa katika daftari la kudumu la wapiga kura ndio wenye haki ya kupiga kura bila ya kuwepo na ubaguzi au bughudha ya aina yoyote. Katika eneo la kupiga kura kunatakiwa kuandaliwe mazingira rafiki yatakayowezesha watu wote kufika kwa urahisi wakiwemo watu wenye ulemavu wa viungo, wasioona, wazee, wanawake wenye watoto na wanawake wajawazito.

5.6: Uzuiaji wa machafuko

Katika mchakato mzima wa uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina mamlaka ya kuhakikisha kipindi cha uchaguzi hakutokei machafuko ya aina yoyote ili uchaguzi ufanyike kwa Amani na uhuru. Tume inaweza kutumia vyombo na taasisi mbali mbali kwa kuwanasihi wananchi kutojiingiza katika mambo yanayopelekea kutokea machafuko. Taasisi za dini pia zinaweza kutumika pia kuzuia machafuko yasitokee na taasisi nyengine za usalama. Vyama vya siasa kutotumia makundi ya vijana kufanya vitendo vinavyoashiria uvunjifu wa Amani.

5.7: Elimu ya mpiga kura

Elimu inayotolewa kwa wapiga kura kuhusu mchakato mzima wa uchaguzi. Elimu hii hutolea na Tume ya uchaguzi. Elimu hii hutolewa kwa njia mbali mbali ikiwa pamoja na kutumia machapicho ya mabango vipeperushi, vajalid, pia vyombo habari hutoa elimu ya mpiga kura kwa kuhabarisha jamii kuweza kutumia haki yao ya msingi na haki ya kikatiba. Taasisi nyengine pia zinaweza kutoa elimu ya mpiga kura ikiwa pamoja na asasi za kiraia zinazoshughulikia masuala ya demokrasia na haki za binadamu.

Kwa upande wa Zanzibar katika kipindi cha uchaguzi taasisi nyingi hujitokeza kutoa elimu ya mpiga kura kwa makundi yote ikiwa ni pamoja na makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Elimu ya mpiga kura hutolewa pia kwa kutumia mitandao ya kijamii, kutumia sanaa ya maigizo na hata tenzi na mashairi.

Muhtasari wa moduli

Uhamasishaji wa jamii ni mchakato wa kuijengea uwezo jamii kupitia wadau wanaofanya kazi na jamii ili kutengeneza mpango wa maendeleo na ushirikishwa wa jamii katika mambo muhimu yenye faida na yanayoweza kuchangia maendeleo kwa jamii husika. Ushirikishwaji huwawezesha wanajamii kuwa na uwajibikaji kuongeza ujuzi na elimu kuhusu mambo mbalimbali yanayohitaji kushughulikiwa na jamii husika kwa maslahi mapana kama vile kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi.

Kuihamasisha na kuishirikisha jamii ni njia bora ya kushughulikia mambo yanayotokea katika jamii na kwa pamoja kushiriki katika kutatua matatizo. Ushiriki huo ni muhimu uzingatie usawa kati ta wanawake na wanaume.

Malengo ya Moduli;

- Kuwawezesha washiriki kufahamu majukumu na dhamana za wadau mbali mbali katika jamii katika kuwasaidia wanawake kweny uchaguzi katika ngazi ya wadi, jimbo na Taifa
- Kufahamu na kuelezea wadau wa kuwasaidia wanawake kuweza kupata ushindi katika nafasi mbali mbali
- Kuweza kuainisha wadau mbali mbali na nafasi na majukumu yao katika ngazi ya jamii watakaoweza kuwa saidia wanawake kupata uongozi katika ngazi ya wadi, jimbo au Taifa
- Kuainisha wada nje ya jamii ambao wataweza kuwasaidia wanawake kuwa viongozi katika ngazi ya wadi, jimbo na Taifa

MODULI YA 4
Majukumu na Wajibu wa Wadau

1.0: Utangulizi

Kwenye mchakato wa uchaguzi kunahitajika kuwa fahamu wadau ambao wataweza kutoa mchango wao katika kuwasaidia wanawake kuwania na kuingia katika kugombea nafasi mbali mbali za uongozi katika ngazi ya wadi, Jimbo au Taifa. Hivyo kunahitajika kuwainisha wadau makundi mbali mbali katika jamii ambao wanatambulikana kuwa wataweza kutumia nafasi yao katika kuwasaidia wanawake kushinda kwenye uchaguzi.

Wadau wa kuwasaidia wanawake katika kupata nafasi ya uongozi ni pamoja na watu binafsi, vikundi, taasisi ambao wanaguswa na masuala ya wanawake kuingia katika nafasi za uongozi katika nafasi za wadi, jimbo au Taifa. Wadau wanweza kuwa wamsingi ambao wana uhusiano moja kwa moja kuathiri au kuathiriwa na ushindi wa wanawake katika uchaguzi na wakiwa sehemu ya jamii wenye taaluma, ujuzi vipaji, uhusiano au rasilimali na wanathaminika katika jamii.

Somo litaanza kwa mwezeshaji kuwauliza masuala washiriki

- Kuainisha makundi mbali mbali ya wadau yatakayoweza kuwasaidia wagombea wanawake kwa nafasi za siasa katika jamii
- Kuoanisha jawabu zitokanazo na bunga bongo na majadiliana mbali mbali

Wadau wanaweza kuwa wanawake, wanaume vijana wafanya biashara, viongozi wa dini na wanajamii wengine. Wadau hawa wanaweza kukuinua au kukuangusha kwa wanasiasa, hivyo ingependeza zaidi majukumu yao katika mchakato yawekwe bayana kwamba ni kuibua changamoto zinazoikabili jamii na changamoto zinazowakabili wanawake kufikia ngazi za uongozi. Wadau hawa wanapaswa watoe mapendekezo kuhusu suluhisho za kutatua vikwazo ili kufikia lengo.

Tunaweza kuweka jedwali la kuonyesha tatizo, sababu ya tatizo, pendekezo la suluhisho na mhusika Mfano:

Tatizo/changamoto	Sababu ya tatizo	Pendekezo/suluhisho	Mdau atakaelishughulikia
Wivu miongoni mwa wanawake wenyewe			
Rasilimali fedha			
Kujiamini			

Kazi ya vikundi: Hii inaweza kufanywa kwa njia ya vikundi kutegemea na idadi ya washirikl. Kwa kuwataka washiriki kuainisha sabau ya tatizo, suluhisho na kuainisha vipi mdau atalishughulikia
Maelezo yatakayopatikana yanaweza kujadiliwa kwa pamoja na baadae mwezeshaji kutoa ufafanuzi kutokana na michango iliyotolewa.

2.0: Majukumu na dhamana ya wadau katika jamii:

i. Vyama vya siasa

Vyama vya siasa ni wadau muhimu katika kuhamasisha na kuwatia moyo wanawake kuchukua/kugombea nafasi za uongozi hasa kwa vile Zanzibar na Tanzania kwa ujumla sheria za uchaguzi zinatambua wagombea kutoka ndani ya vyama vya siasa tu.

- Hivyo vyama vya siasa vinatakiwa kuzuia kut
- umika kwa vitendo viovu au mbinu za udanganyifu, udhalilishaji na rushwa wakati wa uchaguzi. Katika kufanya uteuzi wa mgombea; chama kiangalie sifa za wagombea na sio kuangalia mgombea anatoka katika familia gani au uwezo wake wa kifedha.

- Vyama vya siasa pia vina wajibu wa kutoa elimu kwa wafuasi wao juu ya uzingatiaji wa jinsia na kuwaeleza wafuasi wao kuwa watu wote wana haki ya kugombea na kuchaguliwa bila ya kujali jinsi yake au anakotoka.

- Muhimu sana vyama vya siasa vinahitaji kuandaa mkakati maalum wa kuwezesha wanawake kugombea na kushinda kwa vile historia na dhuluma zimewatendea vibaya kwa miaka mingi nyuma. Viwatengee fedha maalum katika michakato mbali mbali na viwe vinatoa ripoti.

- Vilevile viongozi wa vyama vya siasa wanahitaji kulifanya suala la wanawake na uongozi kuwa ni ajenda yao na hivyo kuisema kila wanapotoa hotuba zao katika majukwaa mbali mbali.

ii. Asasi za Kiraia

Asasi zinafanya shughuli nyingi zinaohusu maendeleo yakiwemo masuala ya demokrasia, kuwezesha wanawake, mabadiliko ya kisheria, haki za binadamu, elimu ya uraia, utawala na haki za watu wenye ulemavu. Asasi za Kiraia ikiwa ni mdau mkubwa wa mchakato wa uchaguzi zina nafasi ya

- Kuainisha na kuhamasisha wanawake kutoka katika kugombea na wanohitaji kusaidiwa hasa yale makundi ya pembezoni yakiwemo wanawake na watu wenye ulemavu
- Kuandaa na kutekeleza mradi utakaosaidia wanawake katika mzunguko mzima wa uchaguzi na kila wakati kukumbushia kupigiwa kura wanawake kwa kutumia nyenzo mbali mbali kama kutneneza vipeperushi na mabango juu mchakato mzima wa uchaguzi ukiwemo uandikishaji
- Kuandaa vipindi vya redio na TV kuhusu masuala ya jinsia na uchaguzi
- Kuandaa makongamano, warsha, mikutano na midahalo yatakayo wainua wanawake kwa kuhamasiha kujitokeza kugombea na kuteuliwa
- Kutumia sanaa kuelimisha jamii na Umma kwa ujumla kuhusu masuala ya wanawake kushiriki katika uchaguzi kwa kujitokeza kugombea na kuchaguliwa.

Asasi za kijamii kama Chama Cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), Umoja wa Wawakilishi Wanawake Zanzibar UWAWAZA, Mwamvuli wa Jinsia Zanzibar (ZGC) , Jumuiya ya Wanawake wenye Ulemavu

Zanzibar (JUWAUZA) ziweke mazingira mazuri ili kuwawezesha wanawake kuwa ni kimbilio wanapofikwa na matatizo katika kipindi chote cha uchaguzi.

iii. **Wanaume wasimamizi wa mabadiliko**

Hili ni kundi maalum la wanaume wanaharakati wapiganiaji wa haki za binadamu. Hawa ni watu ambao wanatambulika na wanaheshimika katika jamii.

Hivyo kazi yao kubwa ni kuchochea mabadiliko kwa wanajamii kwa ujumla na hususan katika jamii ambazo mfumo kandamizi umetawala.

Wanaume wasimamizi wa mabadiliko wanahitaji kutumia ujuzi wao kuhusu masuala ya jinsia na maendeleo kuishawishi jamii kuhusu kumpa mwanamke nafasi ya kugombea uongozi, kumuunga mkono na kuhakikisha kwamba anaondolewa vikwazo ili afikie lengo.

Hivyo wanaume wasimamizi wa mabadilko wanapaswa kuanzisha midahalo na kupitia makundi kwa makundi ili kuleta mabadilko yanayohitajika.

iv. Wanawake

Iwapo wanawake watashikamana kumsaidia mwanamke mwenzao na kuondosha tafauti zao itampa nafasi nzuri mgombea mwanamke hasa tukizingatia wanawake ni wengi katika jamii, ndio wanaojitokeza kwa wingi kujiandikisha, kushiriki kwenye mikutano ya kampeni na kupiga kura. Kadhalika wanawake wapeane moyo na waandae mitandao mbali mbali na wajitokeze kugombea nafasi za uongozi.

Kutoipa nafasi dhana ya kuwa wanawake hawapendani kwani hiyo ni dhana iliyojengwa na mfumo dume, hivyo wanawake wanapaswa waonyeshe kuwa hiyo ni dhana mgando, si dhana ya kimaendeleo kwa kuwashajiisha wanawake kugombea na kuchochea mabadiliko katika jamii na ndani ya vyama vya siasa.

v. Viongozi wa Dini

Hawa ni watu wanaosikilizwa sana na jamii. Wanaweza kutumia nafasi yao kuondosha mitazamo hasi juu ya mwanamke ambayo mingi yao imesambazwa na baadhi ya viongozi wa dini. Kwa mfano katika Uislam wanaume na wanawake wana nafasi sawa katika ibada na pia katika dhana nzima ya uchamungu, hivyo ni wazi kuwa hata katika uongozi wanawake wanayo nafasi yao. Iwapo viongozi wa dini watatumia majukwaa yao kuelezea jinsi mwanamke katika Uislam mathalan; alivyoshiriki katika harakati mbalimbali za kuendeleza jamii na hata alivyoshiriki katika kutoa uamuzi, itasaidia sana kuondosha fikra mgando juu ya wanawake. Hivyo viongozi wa dini watumie majukwaa mbali mbali ikiwemo misikiti, madrasa na makanisa ili kuondosha mawazo hasi dhidi ya wanawake na kuwashajiisha waumini wao wawapigie kura wanawake ili kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

vi. Vyombo vya habari na waandishi wa habari

Vyombo vya habari, Magazeti, TV na Redio ya Umma na binafsi ni wadau makini wa vinaweza kutumiwa kuwahabarisha Umma na kuwajuza na kuelimisha wapiga kura juu ya masuala ya umuhimu wa wanawake kugombea nafasi za siasa katika ngazi za wadi, jimbo au Taifa. Wasikilizaji na watazamaji wa TV wa kawaida wanatabia ya kuwahabarisha wengine taarifa waliozisoma, kusikia na kuona hivyo wananchi wengi watakapoeleimika kuhusu wanwawake kugombea na kuchaguliwa wanawake wagombea watakuwa na nafasi nzuri ya kushinda.

Vyombo vya habari vina wajibu mkubwa katika kuelimisha Umma kwa kutuma mikakati mbalimbali juu ya tarifa sahihi zinazohusu masuala ya mchakato mzima wa wanawake na uchaguzi. Vyombo vya Habari vina nafasi ya;

- Kuelimisha umma kwa kumtumia mhariri kuelezea juu ya masuala ya wanawake na uchaguzi.
- Kuandaa kongamano la waandishi wa habari na kuonyesha uwezo alionao mwanmke anaposhika nafasi ya uongozi
- Kulifanya suala la wanawake kugombea na kushinda katika uchaguzi kuwa ni agenda yao muhimu
- Kuandaa habari, maoni, muhtasari, makala zinazohamasisha wanawake kuingia katika uchaguzi
- Kuandaa wasifu (profiles) za wanawake waliofanya vizuri katika uongozi katika ngazi mbali mbali
- Kufanya uchambuzi wa mara kwa mara kuhusu wanawake katika uchaguzi na kulinganisha na mikataba ya kimataifa, kikanda na kuonyesha rikodi za wanawake wa nchi mbali mbali walioshika nafasi za juu za kisiasa na kufanya vizuri.

Baada ya mada kuwasilishwa mwezeshaji

- Awatake washiriki kuonyesha majukumu mengine ya wadau yatakayoweza kuwasaidia wanawake kushinda uongozi katika ngazi mbali mbali
- Mwezeshaji pia anaweza kuwauliza washiriki kutaja wadau wengine na majukumu yao ambayo wataweza kufanya ili kuwasaidia wanawake kushinda uchaguzi
- Mwisho kufanyike majadiliano na kuoanisha yaliyojitokeza na kutoa suluhisho.

MAREJEO

Chinkin, Christine (2003) Peace agreements as a means for promoting gender equality and ensuring participation of women.

Fair, Laura (1994). Pastimes and Politics, A social History of Zanzibar, Ng'ambo Community: 1890-1950. PhD Dissertation submitted to University of Minnesota, USA.

Richard Strickland and. Nata Duvvury. A Disussion Paper. Page 2. Copyright©2003 International Center for Research on Women.

PARCE-NET: A Gender Transformative Manual for Grassroots Engagement Towards Women Political Empowerment in Malawi (2009)

Women and Leadersdhip in Islam – A Critical Analysis of Classical Islamic – Dr Yussuf Qardhawy

Wajibu wa Jeshi la Polisi katika Chaguzi za Kidemokrasia. Programu ya Mafunzo Inayohusu Haki za Binadamu, Jinsia na Wajibu wa Jeshi la Polisi Katika Uchaguzi wa Kidemokrasia Mwaka 2015

Roman Loimeier (2009) Between Social Skill and Marketable Skills
The Politics of Islamic Education in 20th Century – Zanzibar

Habari Leo (24/11/2013): Dr Ziddy: Uislam hauzuii mwanamke kuongoza

Katiba ya Zanzibar, 1984

CEDAW

MKUZA

Dira ya maendeleo 2020

Sera ya Jinsia, Zanzibar, 2014